# *Kiongozi*

Bwana akubariki, Ndugu Neville. Nina furaha sana kurudi kanisani usiku wa leo. Nimepwelewa tu kidogo na sauti. Kwa namna fulani ulikuwa Ujumbe mrefu asubuhi ya leo, nami kwa kweli nina furaha umekwisha fika, hata hivyo. Nami ninaufurahia, kuutoa, basi ninatumaini mlifurahi kuusikia.

2 Msisahau sasa, daima kumbukeni jambo hili, ya kwamba haya ndiyo mambo yanayomjenga mtumishi wa Kristo. Mnaona, imani kwanza, halafu nguvu. Basi sasa kumbukeni, Roho Mtakatifu hawezi kulitia jengo la Mungu kifuniko mpaka mambo haya yafanye kazi kwa Roho. Mnaona? Hata ufanye nini, mnaona. Hayo ndiyo mambo yanayoujenga Mwili wa Kristo, mnaona, mambo hayo. Naam, msisahau jambo hilo, kwamba hili *hapa* ndilo la kwanza, ni imani yako; nguvu, maarifa, na kadhalika, vinapaswa kuongezwa kwake, mpaka kimo kamili cha Kristo kimedhihirishwa, ndipo Roho Mtakatifu anakuja juu yake na kuutia muhuri kama Mwili mmoja. Vitu hivi havina budi kuwepo. Kwa hiyo, Yesu alisema, "Kwa tunda lao wanajulikana." Mnaona, tunda! Usingeweza kuzaa tunda bila ya mambo haya kulizaa ndani yako. Basi wakati haya yote yanapochukua mahali pa kuupenda ulimwengu na—na kutomcha Mungu, na kadhalika, basi kutokuamini kote kunatupwa nje, ndipo mambo yote ya ulimwengu yamekwisha, basi hapana kitu ila kiumbe kipya katika Kristo. Ndipo Waefeso 4:30 inasema, "Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye Kwaye mlitiwa Muhuri hata siku ya ukombozi wenu." Kutiwa muhuri katika Ufalme wa Mungu! Sasa, msisahau jambo hilo. Tunzeni hilo moyoni mwenu sasa, kunahitajiwa vitu *hivi* kwanza. Halafu kutia muhuri ni Roho Mtakatifu, kile Kifuniko kinachotufunika katika ule Mwili. Vema.

3 Tuna o—ombi sasa kwa ajili ya Dada Little, wa Chicago, mumewe amekuwa katika ajali ya motokaa naye yuko kitandani na ni mahututi sana, Dada Little. Naye Edith Wright, maskini dada yetu hapa ambaye tumemjua kwa muda mrefu sana, yeye ni mahututi sana, sana, yuko nyumbani kwake usiku wa leo, nao walitaka kutangaza jambo hili kanisani ili kwamba sote tupate kuombea haja hii. Basi sasa hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu.

4 Baba yetu wa thamani, wa Mbinguni, tunakusanyika kukizunguka (kwa imani) Kiti cha Enzi cha Mungu, nasi tunaomba rehema ya Kiungu kwa ajili ya haja hizi. Ndugu Little, ajali ya motokaa, mahututi sana. Mungu, msaidie. Jalia kwamba Roho Mtakatifu awe karibu na kitanda chake na amrudishe kwetu, Bwana. Pia maskini Edith Wright kule chini, naomba, Mungu, kwamba Roho Mtakatifu atakuwa karibu na kitanda

chake usiku huu na atamrudishia afya yake tena. Tujalie jambo hilo, Baba. Wewe umeahidi mambo haya, nasi tunayaamini. Na kama tulivyokuwa tunafikiri asubuhi ya leo, ya kwamba umbali si kitu Kwako, Wewe ni mkuu vile vile sehemu moja ya dunia kama ulivyo kwenye ile nyingine, kwa maana Wewe upo kila mahali, una nguvu zote, na huna kikomo. Nasi tunaomba, Baba, ya kwamba utatujalia haja hizi katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

5 Ni furaha sana kuwa humu usiku wa leo tena, pia. Nami najua ya kwamba kuna joto. Hii ni mikutano mitatu mfululizo, na ni. . .Ninajua wengine wenu mna yapata maili mia tano ya kuendesha motokaa kati ya sasa na asubuhi. Na kuanzia kesho kutwa, nina elfu moja mia nne za kuendesha gari baada ya mkutano huo. Kwa hiyo, kwa hiyo mimi—mimi ninatumaini ya kwamba umekuwa wakati mkuu kwenu nyote. Nao umekuwa ni wakati mkuu kwangu kuwazuru. Kuna jambo moja tu ambalo tumeomba, wengi sana imelazimu kurudishwa kwa maana hakuna nafasi, hatuwezi kuyajaza marefu ya kanisa kupita kiasi, zimamoto hawatavumilia jambo hilo. Kwa hiyo tunajaribu sasa kupata kanisa kubwa kidogo, ili kwamba wakati tumeingia, basi tunaweza kuwa na nafasi ya kuketi watu.

6 Basi sasa, wakati wo wote, daima mnakaribishwa hapa maskanini, ambapo hatuna kanuni ya imani ila Kristo, hatuna sheria ila upendo, hatuna kitabu ila Biblia. Na kwa hiyo. . . Na mchungaji wetu ni Ndugu Orman Neville hapa. Nasi tuna kusanyiko hapa la—la watu wengi wanaokusanyika kama maskani isiyobagua madhehebu, mahali unapokuja na kumwabudu Mungu kulingana na maamuzi ya dhamiri yako mwenyewe. Daima tunafurahi kuwa pamoja nanyi. Na kwa hiyo njoni kila mwezapo, daima tuna furaha kuwapokea.

7 Na sasa wakati mwingine, kadiri nijuavyo mimi, kuwa pamoja nanyi, itakuwa ni baada ya kumaliza kanisa. Nami nataka basi, baada ya zile *Nyakati Za Kanisa*, tunataka basi kuziendea zile *Muhuri* saba za mwisho, na zile Muhuri saba za mwisho katika Kitabu cha Ufunuo, kufundisha jambo Hilo.

8 Basi sasa kuna mara nyingi sana ambapo wagonjwa na wanaoteseka huja, na wakati wa mikutano hii, ambapo maono yanahitajika, na kuja kwa ajili ya mazungumzo maalumu ya faragha. Kama nikiingilia jambo hilo, basi mimi—mimi siwezi kamwe kupata tofauti kati yao, na, mwajua, ni vigumu kwangu kuzungumza baada ya jambo hilo. Basi kila mtu anajua ya kwamba katika kampeni zetu za kuponya, ya kwamba Bw. Baxter ama mtu fulani kwa kawaida huhubiri, nami ninatoka kuja kuwaombea wagonjwa, kwa maana ni vigumu kidogo. Nami nilikuwa nikiwaombea watu fulani muda kidogo uliopita, ndipo nikakutana na mtoto mdogo hapa ambaye madaktari. . .kitu fulani mgongoni mwake, alizaliwa kwa njia fulani. Nilipokuwa natoka nje, nilimwona ameketi pale akiwa na plasta. Mtoto huyo

haitambidi kuwa kiwete namna hiyo, atapona. Kweli atapona. Mnaona. Hiyo ni, najua hilo. Unaona, nina hakika na jambo hilo. Kwa hiyo tunataka kuwa na imani yetu na kumwamini Mungu.

9 Kila mmoja wenu, na wengi wenu ni wageni kwangu, wahudumu wote na kadhalika. Kama sijakosea, huyu ni Ndugu Crase. Hiyo ni kweli? Ndugu Crase, na—naomba uniwie radhi, kwa kutofika kule kwa ajili ya kuweka wakfu. Labda nitakuja kule kwa ajili ya mkutano wa mwisho wa juma, itakuwa ni sawa vile vile. Hiyo ni kweli? Huko Bloomington. Mko salama? Vema. Baadhi ya hawa ndugu hapa ni wahudumu, nadhani. Wewe ni mhudumu? Naam, bwana. Bwana awabariki. Basi ni wahudumu wangapi waliomo humu jengoni, hebu tuone mkono wenu. Vema, hilo ni sawa tu. Tunafurahi kuwa nanyi hapa, tuna furaha sana. Mungu awabariki daima!

10 Naam, ili kwamba tuweze kutoka mapema sana, baadhi yao wanaenda Georgia, Tennessee, New York, kila mahali, tangu usiku wa leo, kuanzia usiku wa leo. Naam, endesheni kwa uangalifu barabarani. Kama ukishikwa na usingizi, hutaki kwenda hotelini, ondoka barabarani ukalale mpaka ume-. . .Hivyo ndivyo ninavyofanya. Mnaona, ondoka tu barabarani ukalale. Usi-, usiendeshe ukiwa na usingizi. Ni jambo baya. Pia, kumbuka, si wewe, ni jamaa huyo mwingine unayepaswa kuangalia. Unaona? Wewe unajua unakoelekea, hujui anakoelekea yeye, kwa hiyo—kwa hiyo huna budi kumwangalia jamaa huyo. Kwa hiyo, hakikisha kwamba uko macho wakati wote, kuangalia jambo hilo.

11 Sasa, nitaka kusoma usiku wa leo sehemu ya Maandiko inayopatikana katika Kitabu cha Yohana Mt. Naam, Maandiko haya machache tunayosoma na ambayo tunayarejea, yanapaswa kutupa msingi wa yale tunayojaribu kusema. Na sikuzote, sijawahi wakati mmoja, kama ninavyopata kukumbuka, sijawahi kuja mimbarani, kujaribu kusema jambo fulani kwa kusema tu. Daima mimi hujaribu kungoja, kukesha, kusoma, kuomba, mpaka ninapojisikia ya kwamba nina jambo fulani ambalo lingeweza kuwasaidia watu. Kama siwezi kuwa msaada, basi hakuna haja ya mimi kusimama hapa, mnaona. Ni, kujaribu kusaidia! Na sasa usiku huu, bila shaka, sehemu kubwa ya kundi letu limeondoka tangu asubuhi ya leo, nao iliwabidi kwenda nyumbani, wengi wao. Lakini, usiku wa leo, niliwaambia kama mngeliendelea kubaki tungejaribu kuwa na mazungumzo ya kama dakika arobaini na tano juu ya jambo fulani ambalo ninatumaini lingetusaidia. Nasi tutaliweka jambo hili msingi kwenye Yohana Mt. sura ya 16, na hebu tuanzie kwenye a—aya ya 7 ya sura ya 16, na tusome mpaka a—aya ya 15.

> *Lakini mimi nawaambia iliyo kweli; yawafaa ninyi mimi niondoke; kwa maana mimi nisipoondoka, huyo Msaidizi hatakuja kwenu; bali mimi nikienda zangu, nitampeleka kwenu.*

*Naye akiisha kuja, huyo atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu.*

*Kwa habari ya dhambi, kwa sababu hawaniamini mimi;*

*Kwa habari ya haki, kwa sababu mimi naenda zangu kwa Baba, wala hamnioni tena;*

*Kwa habari ya hukumu, kwa sababu yule mkuu wa ulimwengu huu amekwisha kuhukumiwa.*

*Hata bado nikali ninayo mengi ya kuwaambia, lakini hamwezi kuyastahimili hivi sasa.*

*Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake.*

*Yeye atanitukuza mimi; kwa kuwa atatwaa katika yaliyo yangu na kuwapasha habari.*

*Na yote aliyo—aliyo nayo Baba ni yangu; kwa hiyo nalisema ya kwamba atatwaa katika yaliyo yangu, na kuwapasheni habari.*

12 Sasa katika aya hii ya 13. "Lakini Yeye atakapokuja huyo Roho wa Kweli, atawaongoza awatie kwenye Kweli yote. Atakapokuja huyo Roho wa Kweli, Yeye atawaongoza awatie kwenye Kweli yote." Kweli ni nini? Neno. "Kwa maana atanena, hatanena kwa shauri Lake Mwenyewe; lakini yote atakayosikia, Yeye atayanena. Yote atakayosikia, atayanena." Kwa maneno mengine, Yeye ndiye atakayefunua jambo hilo, mnaona. Na sura ya 4 ya Waebrania, Biblia ilisema ya kwamba "Neno la Mungu ni kali, lina nguvu kuliko upanga ukatao kuwili, Hu—Huyatambua mawazo ya roho, ya moyo." Mnaona, "Yote atakayosikia, atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari zake." Mnaona? Ni kitu gani kitakachofanya jambo hilo? Roho Mtakatifu atakayekuja katika Jina la Bwana Yesu.

13 Nami ningetaka kuchukua dakika hizi nyingine chache zifuatazo kuuvuta usikivu wenu juu ya neno "kuongoza," *Kiongozi*. Mwajua, mimi nimepata ujuzi wa kutosha kiasi huko mwituni. Kiongozi, mtu wa kukuonyesha kila mahali. Huna budi kuwa na kiongozi wakati hujui unakoenda. Nami nikiwa nimezoea kuwinda, na kila mahali ulimwenguni, nimekuwa na na—wasaa wa kukutana na viongozi. Nami ni kiongozi, mimi mwenyewe, huko Colorado, kwa kuwa kwa kuijua hiyo nchi, mambo ya ranchi, na kadhalika, ninaweza kuongoza huko Colorado.

14 Basi, kiongozi hana budi kujua njia. Hana budi kujua anakoenda na anachofanya, na jinsi ya kukulinda njiani. Mnaona? Inambidi kuona ya kwamba hupotei. Kiongozi ni mtu

aliyechaguliwa. Serikali humchagua mtu huyu kama yeye ni kiongozi. Basi, sasa, katika kwenda katika safari ya nyikani, mahali ambapo labda wewe hujazoea kwenda, si jambo zuri kwako kwenda bila mmoja. Kwa kweli, sehemu nyingine hata huwezi kwenda bila mmoja, kwa mfano, Canada. Huyo—huyo kiongozi hana budi kutia sahihi leseni yako kwa mlinzi wa wanyama pori. Hana budi kutia sahihi mwenyewe, naye ana wajibu wa kukulinda. Iwapo kitu cho chote kitakupata, ni wajibu wake. Hana budi kukushughulikia. Inampasa aangalie ya kwamba hupotei. Hana budi kuhakikisha ya kwamba hakutumi mahali fulani ambapo hujui njia ya kurudi. Nawe ukipotea, inampasa kujua hiyo nchi vema sana hata anaweza kukuokota wakati wo wote tu. Inampasa kujua mambo haya yote la sivyo hawezi kuwa kiongozi, hawezi kupewa leseni ya kuwa kiongozi.

15 Kwa mambo haya, mara kwa mara huna budi kuwa na maafikiano, uwasiliane kwanza kwa simu na kufanya matayarisho, ujiwekee mipango ya kupelekwa huko nje. Basi kama nini hii yako . . . Wakati mwingine yeye hana nafasi na hawezi kukuchukua, huna budi kuahirisha jambo hilo kwa muda, kwa—kwa kiongozi wa duniani. Haikubidi kamwe kufanya jambo hilo na Kiongozi wa Mungu, Yeye daima yu tayari, daima yu tayari.

16 Naam, kama hufanyi matayarisho haya, nawe unawazia kufanya safari ya kwenda matembezini porini ambako hujapata kuwa kule bado, huenda ukapotea, na uangamie. Una nafasi ya kama asilimia moja ya kutoka huko porini, hiyo ni kusema, kama si nene sana, huenda ukawa na nafasi ya asilimia moja ya kutoka wewe mwenyewe. Lakini kama ni pori baya sana, huko mbali sana, haiwezekani kwako kutoka. Hakuna njia ya kufanya jambo hilo, kwa maana utajikuta kwenye mkondo wa mauti, halafu ume—umekwisha, basi umekwisha. Naam, nawe utaangamia kama huna kiongozi anayejua hiyo nchi na anayejua namna ya kurudi.

17 Wengi wenu mnazo habari za nakala mliyosoma mwaka jana kutoka Tucson, Arizona, hao Maskauti Wavulana. Hata hivyo, wao walikuwa wamefunzwa jinsi ya kujishughulikia, walikuwa maskauti. Nao hawakuwa Maskauti wa Klabu tu, walikuwa maskauti kamili. Basi walienda safari fupi ya kupanda milima, ndipo mvua kubwa ya theluji ikaja, maumbile yakabadilisha mahali pake. Basi sababu ya kujikuta wamepotea na wote wameangamia, ni kwa sababu wao . . . kitu fulani, badiliko huja nje ya utaratibu wa kawaida, hawakujua jinsi ya kutoka. Mnaona? Nami nasahau ni wavulana wangapi walioangamia huko mlimani, ingawa walituma huko mahelikopta, na Jeshi la Mgambo, na Walinzi wa Taifa, na watu wa kujitolea, na kadhalika. Lakini walipotea, hakuna anayejua walikuwa wapi. Nao hawakuweza kujishughulikia. Wote waliangamia katika theluji kwa kuwa hawakujua kama walikuwa wanaelekea

mashariki, kaskazini, magharibi au kusini, juu ama chini, ama jinsi ilivyokuwa, kila kitu kilifanana.

18 Naam, kiongozi anajua mahali alipo, hata hali ya hewa iweje. Yeye—yeye ameandaliwa ili atekeleze jambo hilo. Anajua analofanya. Yeye ana ujuzi na kila kitu. Anajua jinsi mambo yote yalivyo, kwa hiyo anaweza tu kuwa gizani na angeweza kuhisi kitu fulani.

19 Kwa mfano, huu hapa ujanja wa kawaida wa kiongozi. Mwajua, kama unaweza kuona nyota, kila mtu unaweza kujua unakoelekea kama utaangalia nyota. Nawe daima unapaswa kuangalia ile nyota moja ya kweli. Kuna nyota moja tu ya kweli, na hiyo ni nyota ya kaskazini. Mnaona, moja pekee, inasimama mahali pale pale. Hiyo inamwakilisha Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele. Wengine huenda wakaondoka, bali Yeye hudumu yeye yule. Makanisa yanaweza kukuelekeza *huku*, ama mengine yakuelekeze *kule*; bali si Yeye, Yeye ni yeye yule daima.

20 Vema, sasa, kama huwezi kuona nyota hii ya kaskazini, na kuna mawingu, basi kama utaangalia, kama ni wakati wa mchana nawe umepotea, kama utaangalia miti. Mti daima, ule ukungu uko upande wa kaskazini wa mti, kwa maana upande wa kusini wa mti unapata jua zaidi ya upande huo wa kaskazini. Lakini vipi kama kuna giza nawe huwezi kuuona huo ukungu? Kama utafunga macho yako wala usijaribu kuwaza lo lote, fumba macho yako na ushike mti wenye maganda laini, uukumbatie huo mti namna *hii* mpaka vidole vyako vikutane, kisha uanze kuuzunguka huo mti polepole sana. Basi utakapofikia mahali ambapo ganda ni nene mno, limekatika-katika, huo ndio upande wa kaskazini (pepo), nawe unaweza kujua unaelekea upande gani, kaskazini ama kusini. Basi kwa njia hiyo, loo, kuna mambo mengi, bali inahitaji viongozi kujua namna ya kufanya mambo hayo. Mtu wa kawaida tu anafika pale na kusema, "Mimi sioni tofauti yo yote katika jambo hilo." Mnaona? Mnaona, huna budi kufunzwa kwa ajili ya kuongoza huko.

21 Nao hawa vijana, hapana shaka ila walikuwa maskauti bora, huenda waliweza kufunga vifundo, huenda waliweza kuwasha moto kwa miamba, na vitu kama hivyo. Bali kujua njia yako ya kutokea, hilo ndilo jambo muhimu! Wao, wao hawakujua njia yao ya kutokea, kwa hiyo basi wote wakaangamia kwa sababu hawakuchukua kiongozi wa kuambatana nao.

22 Baba fulani asiyejali, miaka miwili iliyopita, huko Colorado, loo, yeye alikuwa anapanda kwenda milimani, alikuwa na kijana mdogo mwenye umri wa kama miaka sita, saba. Alikuwa anataka kumpeleka kuwinda kulungu kwa mara yake ya kwanza. Kwa hiyo wakapanda juu mlimani, ndipo huyo mvulana mdogo akamwambia babaye, "Ninachoka."

23 “Panda mgongoni mwangu. Hatujapanda juu vya kutosha bado, kulungu wako juu.” Huyo mtu akaendelea na kuendelea na kuendelea kupanda mpaka akafika . . . Yeye hakujua, alikuwa mtu wa mjini. Hakujua cho chote kuhusu kuwinda ama mahali pa kwenda. Mtu ye yote anayejua cho chote juu ya pori anajua ya kwamba kulungu hawakai kule juu. Wao hawapandi huko juu. Mbuzi hukaa kule juu, si kulungu. Wao wako kule chini wanakoweza kula, hawana budi kwenda mahali palipo na kitu cha kula. Na, kwa hiyo, bali mtu huyu alifikiri, “Kama nikipanda huko juu kabisa kwenye miamba mahali fulani huko juu, nitapata dume kubwa la kulungu.” Alikuwa ameona picha ya wengine waliosimama juu—waliosimama juu ya mwamba, naye akafikiri huko ndiko angempata. Msijali yanayosema magazeti hayo, jamani, loo, jamani, utapatwa na jinamizi! Hilo, kuna jambo moja tu la kufanya, ni kumchukua kiongozi ambapo utajua mahali ulipo.

24 Basi baba huyo, ikaja mvua mara moja kule juu, moja ya hizo mvua za haraka zinazokuja. Naye huyo mtu aliwinda akiwa amechelewa mno, hata ikawa giza naye asingeweza kuona njia yake ya kurudia. Kisha hizo . . . kisha pepo zikaja kutoka ng’ambo ya vilele vya ile milima, na huku yeye mwenyewe anatembea haraka, na hilo . . .

25 Huna budi kujua jinsi ya kupona hatarini, kama umekwama. Kuna jambo jingine, ujue jinsi ya kujihami! Nimepanda juu ya miti na kushuka miti kwa kujitelezesha, nikapanda miti kisha nikajitelezesha kushuka, juu chini namna hiyo, nipate kuendelea kuishi. Nimeingilia theluji wakati ingekuwa futi nne kila upande, nikapasua kisiki na kukiweka chini. Nami nina njaa sana hata ilikuwa vigumu kuistahimili! Basi ninapasua hivi visiki vichakavu, na kuviwasha moto na kuviacha vipate moto na kuyeyusha ile theluji. Na halafu kama saa saba za usiku, saa nane, ninaviondoa hivyo visiki, kisha nalala kwenye mahali hapo penye joto, niendelee kuishi. Nawe huna budi kujua jinsi ya kufanya mambo haya.

26 Basi mtu huyu hakujua alilokuwa anafanya, hakuwa na mtu pamoja naye wa kumwongoza. Basi akamkumbatia mwanawe mdogo kwenye kifua chake mpaka akamsikia anapoa kwa baridi kisha akafa. Kutokujali! Kama angalienda tu na kiongozi, yeye angaliweza kumshusha moja kwa moja mlimani haidhuru ilikuwa ni wakati gani, mnaona. Bali yeye alingoja mpaka ikawa giza, ndipo hakuweza kuona njia.

27 Hiyo ndiyo shida ya Wakristo leo. Wao wanangojea mpaka giza linaingia, ndipo unapata kwamba umeondoka bila Kiongozi. Kiongozi!

28 Ati, ulipata kuona mtu aliyepotea? Kuna mtu aliyepata kuwa na tukio la kumrudisha mtu aliyepotea? Ni jambo la kuhuzunisha sana ulilopata kuona. Mtu anapopotea, anakuwa

mkaidi. Hajui analofanya. Tulimpata mtu huko nje, mvulana, naye alikuwa amepotea mwituni, naye alidhaniwa. . . Yeye alikuwa mchungaji, bali alikuwa katika jimbo lingine naye akapotea, akazungukazunguka. Nao walipompata siku tatu baadaye, alikuwa anakimbia kama mtu mwenye kichaa, akipiga makelele kwa nguvu zake zote. Midomo yake ilikuwa imeliwa yote, basi akatupa bunduki yake na hakujua la kufanya. Na wakati ndugu yake mwenyewe, wakati. . . Iliwabidi kumshika na kumfunga. Wakati ndugu yake mwenyewe alipomjia, alipigana naye kama mnyama, akajaribu kumuuma, hakujua yuko wapi. Kwa nini? Alikuwa amepotea. Basi wakati mtu anapopotea, yuko katika hali ya kufadhaika. Wala hajui ya kwamba yuko katika hali hiyo, kwa kuwa kupotea kwake kunamletea fadhaa hii, wala hajui aliko na jinsi anavyotenda.

29 Ndivyo ilivyo wakati mtu amepotea kutoka kwa Mungu! Yeye atafanya mambo ambayo kwa kawaida asingaliyatenda. Atafanya mambo ambayo—ambayo yamepita fikara za mwanadamu kufanya. Mtu aliyepotea kutoka kwa Mungu, kanisa lililopotea kutoka kwa Mungu, kanisa lililomwacha Mungu, lililoondoka kutoka kwenye kanuni za Biblia ya Mungu, litafanya mambo ambayo wakati mwingine kwamba usingetarajia kuyaona katika kanisa la Mungu aliye hai. Wao watachuma fedha zao kwa mchezo wa kamali, kucheza karata, bahati nasibu, cho chote wanachoweza kufanya. Watafundisha cho chote, wataachilia cho chote kile, wawapongeze watu ambao wanatoa sana kanisani, na kadhalika namna hiyo, kuwaacha wakubaliwe kwa jambo hilo. Hiyo ni kweli. Wawaweke mashemasi kwenye halmashauri ambao wameoa mara nne ama mara tano, ili kwamba tu wapate kukubaliwa, wapate kufanikiwa. Kuna ufanisi mmoja tu unaopaswa kufanikisha, huo ni, wajibu wako kwa Mungu. Simama na useme Kweli! Kupotea, mtu aliyepotea yuko katika hali ya fadhaa, yeye ni mwenda wazimu.

30 Kiongozi anaelewa, jinsi ya kwenda na jambo gani la kutenda. Mungu katika. . . Mungu daima amewatumia watu Wake kiongozi. Mungu hajashindwa kamwe. Yeye hutuma kiongozi, bali huna budi kumkubali kiongozi huyo. Mnaona? Huna budi kuamini jambo hilo. Huna budi kupitia njia anayosema. Kama ukiingia nyikani, naye kiongozi wako anasema "tunaenda *hivi*," na hata hivyo unafikiri unaenda *vile*, mwishowe utapotea. Basi unapo-. . . Mungu anapotutumia kiongozi kutuongoza, hatuna budi kumfuata kiongozi huyo. Haidhuru tunafikiri nini, yale yanayoonekana ni ya maana na ambayo yanaonekana hayasadikiki, hatuwezi kupambanua jambo hilo, kiongozi ndiye tu anayeweza.

31 Mungu, katika Agano la Kale, aliwatuma manabii. Wao walikuwa viongozi, kwa maana Neno la Bwana liliwajilia manabii. Wao walikuwa viongozi. Waliwafundisha watu kama

tulivyosema jana usiku, juu ya Isaya na Uzia. Wao walifunzwa, nao waliwafunza watu na kuwaongoza. Na sasa Mungu daima amewatuma viongozi Wake, Yeye daima hajakosa kuwa na kiongozi, katika nyakati zote. Mungu daima amekuwa na mtu fulani aliyemwakilisha katika dunia hii, katika nyakati zote.

32 Naam, mara kwa mara wanamwacha kiongozi, "nje ya mstari," kama tunavyosema. Wakati Yesu alipokuwa hapa duniani, hivi hamkumbuki Yesu aliwaambia Mafarisayo, "Enyi viongozi vipofu"? Viongozi vipofu, vipofu kwa mambo ya kiroho. Mnaona? Naam, walidhaniwa kuwa ni viongozi, viongozi wa watu, wakiwaongoza watu kwenye wokovu. Lakini Yesu alisema, "Ninyi ni vipofu!" Kisha akasema, "Waacheni, kwa maana kama kipofu akimwongoza kipofu, je! wote wawili hawatatumbukia shimoni?" Viongozi vipofu! Loo, jinsi ulimwengu ulivyochafuliwa na huo, uongozi mpofu! Yeye hataki wewe utegemee akili zako mwenyewe. Mungu hataki wewe utegemee akili zako mwenyewe ama mawazo yako mwenyewe, wala mawazo ya kujibunia.

33 Mungu hutuma Kiongozi, naye Mungu anataka mkumbuke ya kwamba huyo ni Kiongozi Wake aliyemchagua. Nasi hatuna budi kumkumbuka Yeye. Hapa linasema, Yesu alisema, "Sitawaacha, bali nitamwomba Baba naye atawatumia Mfariji mwingine." Naye huyu Mfariji, alipokuwa aje, ilikuwa atuongoze kwenye Kweli yote. Nalo Neno la Mungu ndilo Kweli, nalo Neno ni Kristo, "Mimi ndimi Njia, Kweli, na Uzima." Yeye ni Neno, "Hapo mwanzo kulikuweko Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili akakaa kwetu." Basi kama tukimfuata yule Kiongozi halisi na wa kweli, Roho Mtakatifu, Yeye alikuwa atwambie aliyokuwa ameona, aliyokuwa amesikia, na alikuwa atupashe habari za mambo yajayo. Amina. Haya basi. Yeye atawaonyesha mambo yajayo.

34 Basi wakati makanisa leo yanakataa jambo Hilo, tunawezaje kutarajia kwenda Mbinguni? Wakati Roho Mtakatifu alitumwa kwetu kuwa Kiongozi, tutamchukua kadinali fulani, askofu fulani, kiongozi mkuu fulani, ama mtu fulani kama huyo kutuongoza, wakati Roho Mtakatifu alitolewa kwetu apate kutuongoza.

35 Naye Roho Mtakatifu daima hunena kuhusu Neno. "Nina mambo mengi ya kuwaambia, hamwezi kuelewa na jambo hilo sasa, bali Yeye ajapo, atawaongoza kwenye Hilo." Hiyo ndiyo sababu ya kuja kwa zile Muhuri. Na katika kumalizia kwa ile Muhuri ya Saba, siri ya Mungu haina budi kutimizwa, kujua Mungu ni nani, Yeye ni nini, jinsi anavyoishi, tabia Yake, Utu Wake. Unapaswa usafiri uje kufikia umbali *huu* ifikapo wakati huo, mnaona, kutuleta katika kimo kikamilifu cha wana na binti za Mungu, Kanisa ambalo limeoshwa katika Damu ya Kristo, lililonunuliwa bila pesa, limelipiwa kwa Damu ya Yesu Kristo.

36 Naam, haya basi, Kiongozi, naye Ndiye Kiongozi aliyetolewa na Mungu. Naam, tunapita katika nyika nasi tumo njiani kuelekea mahali fulani, nasi hatuwezi kuendelea bila Kiongozi huyu. Na mtu ye yote athubutu kuweka kiongozi ye yote yule mahali pake! Kama ukifanya jambo hilo, yeye atakuondoa njiani. Kiongozi huyu anajua njia! Yeye anajua kila inchi ya hiyo njia. Anajua kila wazo lililo moyoni mwako. Anamjua kila mtu aliye hapa. Anajua wewe ni nani na umefanya nini, na kila kitu kukuhusu wewe. Yeye ni Kiongozi wa Mungu, Roho Mtakatifu, naye atakufunulia mambo, pia atakuambia mambo aliyosikia, anaweza kurudia maneno yako moja kwa moja na kusema uliyosema. Amina. Kukwambia ulivyokuwa, uliyo nayo, mahali unakoelekea. Kiongozi, Kiongozi wa kweli, naye atakuongoza akutie kwenye Kweli yote, na Neno Lake ndiyo Kweli.

37 Naam, Roho Mtakatifu hatakufanya kamwe, useme "amina" kwa namna fulani ya kanuni ya imani ya kujibunia. Ataitikia tu Neno la Mungu kwa "Amina," maana ndivyo lilivyo. Roho Mtakatifu hatakuongoza njia nyingine yo yote. Sasa jambo la kushangaza ni kwamba, ya kwamba sisi sote, madhehebu yetu yote makuu na kadhalika, tunadai kila moja linaongozwa na Roho Mtakatifu, na kuna tofauti kubwa kama kulivyo katika mchana na usiku katika sisi wote.

38 Lakini wakati Paulo, maskini Mfarisayo huyo aliyempokea Roho Mtakatifu wakati Anania alipombatiza, kisha akaenda Arabuni na kujifunza kwa miaka mitatu, akarudi, wala kamwe hakulitaka shauri kanisa juu ya jambo lo lote kwa miaka kumi na minne, naye alipokuja na kukutana na Petro, kiongozi wa kanisa huko Yerusalemu, walipatana kabisa katika Mafundisho. Kwa nini? Roho Mtakatifu yule yule! Mahali ambapo Petro alibatiza katika Jina la Yesu Kristo, Paulo alifanya jambo lile lile bila ya mtu ye yote kumwambia. Mahali ambapo Petro alifundisha ubatizo wa Roho Mtakatifu, na utakaso, na kadhalika; Paulo alifanya jambo lile lile, bila ya kulitaka shauri kanisa, kwa sababu ilikuwa ni Kiongozi yule yule. Basi sisi tunaweza kuwa wapi leo wakati watu wanakana Kweli hizi? Wakati Petro alipofundisha alichofundisha kuhusu jinsi kanisa lilivyokuwa liwekwe katika utaratibu, Paulo alikuwa na Fundisho lile lile, maana wao walikuwa na Kiongozi yule yule.

39 Kiongozi hatampeleka mmoja *huku*, na mwingine *kule*, na kumtuma mmoja mashariki na mwingine magharibi. Yeye atawaweka ninyi pamoja. Na kama tutamwacha tu Roho Mtakatifu atuweke pamoja, tutakuwa mmoja. Kama—kama tu hatutamwacha Ibilisi akuvutie kwenye barabara mbaya, tutakuwa na moyo mmoja, nia moja, na katika umoja, kwa Roho Mmoja, Roho Mtakatifu, Kiongozi wa Mungu atakayetuongoza atutie kwenye Kweli yote. Hiyo ni kweli. Lakini huna budi kumfuata Kiongozi wako. Naam, bwana.

40 Mwangalie Nikodemo, yeye alihitaji Kiongozi, hata hivyo alikuwa mtu mwerevu. Alikuwa mwalimu, mwenye umri wa kama miaka themanini. Alikuwa wa Mafarisayo, ama—ama Baraza la Wazee, lile Baraza, Halmashauri ya Wahudumu. Alikuwa mmoja wa watu wao walio maarufu kuliko wote, mwalimu katika Israeli, hodari kwa jambo hilo. Wazieni, mwalimu hodari! Naam, yeye alijua torati, bali ilipofikia kwenye kuzaliwa mara ya pili, alihitaji Kiongozi. Alikuwa anamwonea njaa. Yeye alijua ilibidi kuwe na kitu tofauti. Aliyomwambia Kristo usiku ule yalithibitisha jambo hilo. Yalithibitisha jambo hili pia, maoni ya wengine wao, bali hakuna mmoja wao aliyekuwa na u—ujasiri aliokuwa nao. Hakuna hata mmoja wao angalikuja kule na kufanya aliyofanya. Mwajua, watu wanamhukumu Nikodemo kwa kuja usiku. Alifika mahali pale. Aliwasili. Ninajua watu fulani ambao hata hawataanza, iwe usiku ama mchana. Bali yeye alifika pale, naye alihitaji Kiongozi, naye akasema, "Bwana, sisi," kutoka Baraza la Wazee, "tunajua ya kwamba Wewe ni Mwalimu uliyetoka kwa Mungu." Kwa nini alijua? Yeye alikuwa amethibitishwa. Mnaona, alitaka kujua maana ya huku kuzaliwa mara ya pili, naye akaenda moja kwa moja kwa Mtu sahihi, kwa maana Mungu alikuwa amethibitisha ya kwamba huyu alikuwa ndiye Kiongozi Wake, Yesu. Angalieni aliyosema, "Bwana, twajua Wewe u Mwalimu uliyetoka kwa Mungu, maana hakuna mtu awezaye kufanya mambo unayofanya Wewe, isipokuwa Mungu yu pamoja naye."

41 Ilikuwa ni thibitisho pale, kwamba kulikuwa na Mungu aliye hai ndani Yake. Yale aliyoshuhudia, "Si Mimi nizifanyaye zile kazi; ni Baba Yangu anayekaa ndani Yangu. Amini nawaambieni, Mwana hawezi kufanya neno kwa nafsi Yake Mwenyewe; bali lile analomwona Baba akifanya, ndilo analofanya Mwana vile vile. Baba anafanya kazi, Nami ninafanya kazi vile vile." Katika maneno mengine, Mungu alimwonyesha la kufanya, naye akatoka akaenda akatenda tu vile vile. Yeye hakufanya neno lo lote hata Mungu alipomwambia afanye. Amina. Hizo ni kweli zake halisi. Kama tu tungeshughulika tu na kungojea mpaka Roho ametuongoza kufanya jambo hilo! Naam basi. Kisha tuingie kabisa katika Kristo hata haimbidi kukusukuma kila mahali kama anavyonisukuma mimi, bali tikiso dogo la kwanza la kichwa Chake, uko tayari na hakuna kitu kitakachokuzuia, kwa sababu unajua ya kwamba ni mapenzi ya Mungu.

42 Yeye alihitaji Kiongozi. Naye alikuwa Kiongozi aliyethibitishwa. Aliweza kuongozwa na Kiongozi huyu kwa sababu alijua Kiongozi huyu aliongozwa na Mungu. Alijua ya kwamba yale mapokeao aliyokuwa ametumikia, labda na Mafarisayo, Masadukayo, na wo wote wale, alikuwa amezitumikia kanuni hizo za imani kila wakati wala hakuona lo lote likitukia. Bali huyu hapa Mtu anatokea hadharani, akisema

ya kwamba Yeye ni Masihi aliyeahidiwa wa Biblia. Kisha anageuka na kufanya kazi zile hasa za Mungu. Yesu alisema, "Kama nisipozifanya kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi. Bali kama hamwezi kuniamini Mimi, aminini kazi zile hasa ninazofanya, kwa maana zinanishuhudia Mimi."

43 Halafu, si ajabu Nikodemo aliweza kusema, "Bwana, tunajua Wewe ni Mwalimu uliyetoka kwa Mungu, kwa maana hakuna mtu awezaye kufanya mambo ufanyayo Wewe bila Mungu kuwa pamoja Naye." Mnaona, yeye alihitaji Kiongozi, ingawa alikuwa hodari wa jambo hilo. Yeye alikuwa mkuu wa kanisa lake. Alikuwa na cheo, naye alikuwa—alikuwa na mahali maarufu, naye alikuwa ni mtu mashuhuri; hapana shaka, aliheshimiwa na watu wote nchini. Bali ilipofikia kuzaliwa mara ya pili, yeye alihitaji Kiongozi! Nasi pia, naam, tulihitaji Kiongozi.

44 Kornelio, yeye alikuwa mtu mashuhuri, mheshimiwa. Alijenga makanisa. Aliwaheshimu Wayahudi kwa maana alijua ya kwamba dini yao ilikuwa ya kweli. Naye alitoa sadaka, naye aliomba kila siku, bali wakati Roho Mtakatifu alipokuja (Kitu Fulani kilikuwa kimeongezwa kwenye kanisa), Yeye alihitaji Kiongozi. Mungu alimtumia Roho Mtakatifu. Alimtuma katika utu wa Petro, "Bali Petro alipokuwa anasema Maneno haya, Roho Mtakatifu akamshukia." [Mahali patupu kwenye kanda—Mh.] Mungu alimtumia Kiongozi kupitia kwa Petro. Alimtumia, kwa sababu Yeye alimwongoza Kornelio kwenye njia sahihi. Basi alipokuwa akinena, Roho Mtakatifu akawashukia hao Mataifa. Ndipo akasema, "Mtu anaweza kukataza maji, kwamba watu hawa wasibatizwe?" Mnaona, Kiongozi angali anazungumza, si Petro. Kwa sababu hilo lilikuwa ni kundi la Wayahudi... ama Mataifa, "najisi, wachafu" kwake, na hata hakutaka kwenda. Lakini yule Kiongozi alisema, "Ninakutuma wewe." Unafanya mambo ambayo hufikiri ungeweza kufanya, wakati yule Kiongozi anapochukua mamlaka yote, unapomwacha Yeye akuongoze. Loo, ni jambo zuri namna gani kuongozwa na Roho Mtakatifu. Yeye ndiye Kiongozi. Vema. Yeye alinena na Petro akamwambia analopaswa kufanya. Ndipo wakati hao wote walipompokea Roho Mtakatifu, yeye alisema, "Hatuwezi kukataza maji, kwa kuwa hawa wamempokea Roho Mtakatifu kama sisi tulivyompokea hapo mwanzo." Basi wakawabatiza katika Jina la Bwana Yesu. Naam, ni nani aliyemwongoza kufanya jambo hilo? Kiongozi aliyekuwa ndani yake. Je! Yesu hakuwaambia, "Msifikirie mtakalosema, maana si ninyi mnaonena; ni Baba anayekaa ndani yenu, Yeye ananena"? Amina.

45 Yule towashi, akishuka kutoka Yerusalemu. Na Mungu alikuwa na Kiongozi duniani wakati huo, Roho Mtakatifu, naye alikuwa na mtu kule chini aliyekuwa amejazwa na Kiongozi huyu. Yeye hata hakuwa mhubiri, alikuwa kwa namna fulani

kama shemasi. Naye alikuwa kule chini akiwaponya wagonjwa na kuwatoa pepo, na kusababisha mwamsho mkubwa, furaha kubwa ilikuwa mjini. Yeye alikuwa amezungukwa na mamia ya watu, ndipo yule Kiongozi akasema, "Hiyo imetosha, hebu turudi hivi." Yeye hakubishana na Kiongozi wake.

46 Usishindane kamwe na Neno la Kiongozi wako. Mfuate Yeye. Kama humfuati, utapotea. Pia, kumbuka, unapomwacha, uko peke yako, kwa hiyo tunataka kuwa karibu na yule Kiongozi.

47 Kwa hiyo humo njiani, Yeye alisema, "Acha kundi hili sasa, Filipo, utoke uende jangwani mahali ambapo hapana mtu. Bali ninakutuma huko, na kutakuweko na mtu nitakapokupeleka kule." Huyu hapa anakuja towashi mpweke, alikuwa mtu mashuhuri kwa yule malkia kule Kushi. Kwa hiyo alikuwa anashuka akija, akisoma Kitabu cha Isaya. Basi yule Kiongozi akasema, "Nenda karibu na lile gari."

Ndipo akasema, "Je! unafahamu unayosoma?"

48 Akasema, "Ninawezaje kufahamu wakati hakuna mtu wa kuniongoza?" Loo, jamani! Bali Filipo alikuwa na yule Kiongozi. Amina. Naye akaanzia kwenye Maandiko yale yale, akamhubiri Kristo. Amina. Kiongozi! Si kumwambia kanuni fulani za imani, yeye alimwambia juu ya Kiongozi, Kristo! Ndipo akambatiza huko nje majini. Hakika, ilikuwa hivyo. Loo, jinsi ninavyopenda jambo hilo!

49 Israeli walipotoka Misri wakienda kwenye ile nchi ya ahadi, katika Kutoka 13:21, Mungu alijua ya kwamba wao hawajapita njia hiyo hapo kabla. Ilikuwa tu maili arobaini, bali hata hivyo walihitaji kitu fulani cha kwenda pamoja nao. Wangepoteza njia yao. Kwa hiyo Yeye, Mungu, akawatumia Kiongozi. Kutoka 13:21, kitu kama hiki, "Ninamtuma Malaika Wangu aende mbele zenu, ile Nguzo ya Moto, ili awalinde njiani," kuwongoza kwenye nchi hii ya ahadi. Nao wana wa Israeli wakamfuata Kiongozi yule, ile Nguzo ya Moto (usiku), Wingu mchana. Wakati iliposimama, wao wakasimama. Wakati iliposafiri, wao wakasafiri. Basi Yeye alipowafikisha karibu na ile nchi, nao hawakuwa wanastahili kuvuka, Yeye aliwaongoza akawarudisha jangwani tena. Asingeenda pamoja nao.

50 Hivyo ndivyo lilivyo, kanisa leo. Hapana shaka ila ni uvumilivu wa Mungu leo, kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, kanisa lingekwisha ondoka kama lingalikuwa limesahihishwa tu na kuwekwa katika utaratibu. Bali Yeye hana budi kuzidi kutuongoza kuzunguka na kuzunguka na kuzunguka.

51 Israeli hawakujua hata kidogo, wakati walipokuwa wanapaza sauti, walipowaona askari waliokuwa wamekufa wa Misri, farasi waliokufa maji, magari ya Farao yamepinduliwa juu chini, wao walipata ushindi, Musa katika Roho, akiimba katika Roho, Miriamu akicheza katika Roho, na binti wa Israeli wakikimbia huku na huko ukingoni, wakipaza sauti na kucheza,

walikuwa siku chache tu kutoka kwenye maziwa na asali. Hawakujua hata kidogo ilikuwa umbali wa miaka arobaini, kwa maana walianza kunung'unika dhidi ya Mungu na yule Kiongozi.

52 Nasi tunajikuta namna ile ile. Nitaenda huko Shreveport baada ya hapa. Naye Roho Mtakatifu alishuka kwenye Siku ya Kutoa Shukrani, miaka hamsini iliyopita, huko—huko Louisiana, kwenye Siku ya Kutoa Shukrani. Jinsi kanisa limeanguka tangu wakati huo! Mnatambua ya kwamba kanisa Katoliki la Kirumi katika mwanzo wake lilikuwa Kanisa la kipentekoste? Hiyo ni kweli. Hiyo ni sawa. Lilikuwa kanisa la kipentekoste, bali hao watu mashuhuri wenye mioyo migumu wakaanza kuingia na kubadilisha Ma—Maandiko ya Mungu kwa mapokeo yao, kuongeza Kwake mafundisho ya sharti, na kadhalika. Basi angalia walicho nacho sasa, hamna hata kipande kidogo cha Maandiko katika hata moja yao. Wao walitia kitu fulani badala ya kitu fulani kingine, kipande cha mkate badala ya Roho Mtakatifu. Waliweka kunyunyizia maji badala ya kuzamisha. Waliweka "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu" badala ya "Bwana Yesu Kristo." Waliondoa maagizo haya yote makuu ya Mungu yaliyowekwa kwa ajili yetu, nao wako mbali, mbali sana, sana na Fundisho la Kimaandiko.

53 Nayo Pentekoste ilishuka Louisiana, miaka hamsini iliyopita, na kama ikisimama miaka mingine mia mbili, itakuwa mbali zaidi kuliko kanisa Katoliki lilivyo, kama likiendelea kuanguka jinsi limeanguka miaka hii hamsini iliyopita, maana wao wanaongeza tu kwake wakati wote, daima. Wale wahubiri wa mtindo wa kale wameondoka. Mikutano ya mitaani, huisikii hata mmoja. Jambo hili lote tulilo nalo ni kundi la Hollywood lililoongezwa mle, wanawake waliokata nywele zao wakivaa kaptura, wamejipodoa, na kila takataka, wakijiita Wakristo. Maskini Ricky fulani mwenye gitaa, anakimbia huku na huko mahali hapo, na wanawake wenye nguo zilizobana sana kama . . . kama tu mnyama aliyechunwa ngozi huku ngo—ngozi imetokeza, karibu imetokeza, wakikatika-katika jukwaani, wakikimbia huku na huko jukwaani, wakicheza huku heleni za maskioni zimening'inia chini, na moja ya mitindo hii mipya hapa ya mfano wa mama-wa-taifa, halafu linajiita lenyewe Ukristo.

54 Tunachohitaji ni dini ya mtindo wa kale, iliyotumwa na Mungu, na inayochoma ambayo itachoma ulimwengu huo wote kutoka kanisani. Tunahitaji kurudi kwenye Roho Mtakatifu na moto, kurudia kile kitu kinachoteketeza takataka, kurudisha mahubiri ya mtindo wa kale, yanayoifanya Mbingu juu, na kuzimu moto, yaliyonyoka kama mtutu wa bunduki. Tunahitaji mahubiri ya namna hiyo. Lakini ukifanya jambo hilo leo, kusanyiko lako litakupigia kura utoke.

55 Mara kwa mara wahubiri wazuri hupotoshwa na kusanyiko lao. Hiyo ndiyo sababu mimi sina madhehebu. Nina makao makuu mamoja, hayo ni kutoka Mbinguni. Po pote anitumapo, nitaenda. Lo lote asemalo, ninasema. Hatutaki madhehebu yo yote. Kanisa hili likithubutu kuzungumza juu ya madhehebu, mmempoteza mchungaji wenu papo hapo. Nisingekaa karibu nalo, si muda mmoja wa dakika tano. Kila kanisa lililopata kufanyika madhehebu lilikufa, basi niambieni moja ambalo halikufa, halafu mniambie moja ambalo lilifufuka tena. Roho Mtakatifu anatumwa kuliongoza kanisa, si kundi fulani la watu. Roho Mtakatifu ndiye hekima yote. Mwanadamu huwa mgumu, asiyejali.

56 Mungu aliwaambia ya kwamba angewatumia Kiongozi, Yeye angewaongoza njiani. Basi mradi tu waliifuata hiyo Nguzo ya Moto, walikuwa sawa. Yeye aliwapandisha akawapeleka mpaka kwenye lango la nchi ya ahadi, na basi huo ndio umbali aliokuwa aende. Ndipo Yoshua, yule shujaa mkuu wa vita, kumbukeni siku aliyowaambia, "Jitakaseni, siku ya tatu Mungu ataufungua Yordani hapa chini nasi tutavuka"? Sasa tazama alilosema (ninapenda jambo hili) katika Maandiko, yeye alisema, "Kaeni karibu nyuma ya lile Sanduku, kwa maana hamjapita njia hii bado."

57 Lile Sanduku lilikuwa ni nini? Neno. Msipitie kwenye njia za madhehebu yenu sasa, kaeni moja kwa moja nyuma ya Neno, maana hamjapita njia hii bado. Basi, ndugu, kama kuliwahi kuwa na wakati ambapo kanisa la Kikristo linapaswa kujichunguza lenyewe, ni sasa hivi. Tuko sasa hivi ambapo mkutano huu mkubwa unaendelea kule Rumi sasa hivi, tofauti zinafanywa, muungano wa Makanisa, ambapo madhehebu haya yote yanaungana pamoja kufanya sanamu ya mnyama, sawasawa hasa na ilivyosema Biblia. Nanyi mnajua tulilosema asubuhi ya leo katika zile Jumbe. Nasi tumewasili, kabisa kila kitu kipo mlangoni, na watu wangali wanafuata kanuni ya imani. Afadhali ukae nyuma ya Neno! Neno litakuongoza hadi ng'ambo ya pili, kwa maana Neno ni Kristo, naye Kristo ni Mungu, naye Mungu ni Roho Mtakatifu.

58 Kaeni nyuma ya Neno! Loo, naam, bwana! Kaeni na Kiongozi huyo. Kaeni vema sawasawa nyuma Yake. Msiende mbele Yake, kaeni nyuma Yake. Hebu Hilo na liwaongoze, msiliongoze. Liachilieni liende.

59 Yoshua alisema, "Naam, hamjapita njia hii bado, hamjui cho chote kuhusu njia hii."

60 Hiyo ndiyo shida leo. Huhitaji kiongozi kukuongoza kushuka kwenye barabara iliyo pana. Loo, unajua njia zote za vichochoro na cho chote kile. Unajua njia yote inayoelekea dhambini. Hakuna. . .Loo, una uzoefu wa muda mrefu sana. Hakuna haja ya mtu fulani kujaribu kukwambia juu ya

jambo hilo, unajua njia zote za mkato. Hiyo ni kweli, kila dhambi, unajua habari zake zote. Hakuna mtu anayepaswa kukwambia namna ya kuiba; unajua hilo. Hakuna mtu anayepaswa kukwambia jinsi ya kulaani; unajua hilo. Hakuna mtu anayepaswa kukwambia namna ya kufanya mambo haya maovu, kwa maana yamewekwa kwenye kila mti kila mahali.

61 Lakini, kumbukeni, ninyi watu mlio Wakristo, mmevuka. Mmeingia katika Nchi nyingine. Mmezaliwa mara ya pili. Mko Nchini, Nchi ya Kimbinguni. Mko kwenye Nchi ya Ahadi.

62 Mnaweza kuangalia, mnajua njia hapa. Loo, jamani, naam. Mnajua nini—nini, jinsi ya kusimama kwenye mkono fulani wa karata. Mnajua dadu, inapofingirika, maana yake ni nini, na kila kitu namna hiyo. Bali inapofikia kujua utakatifu na haki na nguvu za Mungu, na jinsi Roho Mtakatifu anavyofanya kazi na yale anayotenda, afadhali mkae karibu kabisa nyuma ya Neno, yule Kiongozi. Mnaona? Hamjapita njia hii bado.

63 Vema, mnasema, "Nilikuwa mtu mwerevu sana, nilikuwa—nilikuwa na digrii mbili chuoni." Afadhali usahau jambo hilo. Naam, bwana.

64 "Nimepitia kwenye seminari." Afadhali usahau jambo hilo. Naam. Afadhali usimame nyuma ya Kiongozi. Mwache akuongoze. Yeye anajua njia; wewe hujui. Hamjapita njia hii bado. "Vema," mnasema, "wamepita."

65 Angalieni kama wamepita. Yesu alisema, "Hao waliopita kwenye njia hii, ishara hizi zitafuatana nao. Jina Langu, watatoa pepo, watanena kwa lugha mpya; ama watashika nyoka ama wanywe vitu vya kufisha, havitawadhuru. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Karibu wote wanalikataa, wanalikana, wanasema hata halijavuviwa. Wao hawamfuati Kiongozi. Wanafuata kanuni za imani za kujibunia. Afadhali mkae moja kwa moja nyuma ya Neno, kwa maana hamjapita njia hii bado, mwajua.

66 Lakini mmezaliwa mara ya pili, nanyi mmezaliwa katika utakatifu. Hamjapita njia hii bado. Mmepi-. . . Kama mkipita njia hii, hamna budi kupitia katika utakatifu, kwa maana ni Nchi mpya, Uzima mpya, watu wapya.

67 Utakuja kanisani na kusikia mtu fulani akiinuka na kupiga makelele, "Mungu atukuzwe! Haleluya!"

68 Mbona, utasema, "Loo, jamani, hawajafanya hivyo kanisani mwangu! Nitaamka na kutoka!" Mnaona? Uwe mwangalifu.

69 Kaeni nyuma ya Neno, sasa, acheni Kiongozi awaongoze. "Atawaongoza awatie kwenye Kweli yote, na kuwafunulia mambo haya niliyowaambieni habari zake. Yeye atawaonyesha jambo hilo. Mambo yajayo atawapasha habari zake," Kiongozi wa kweli. Usiende kwa askofu; nenda kwa Kiongozi. Usimwendee mtu ye yote ila yule Kiongozi. Yeye ndiye

aliyetumwa kukuongoza. Yeye ndiye atakayefanya jambo hilo. Mungu amewapa Kiongozi. Chukua njia iliyoandaliwa na Mungu.

70 Shida ya jambo hilo leo, ni kwamba watu wanaokuja kanisani wanaketi tu dakika chache, jambo fulani linaendelea ambalo wao hawajazoea.

71 Nilimpenda maskini mwanamke fulani kutoka kwenye kanisa baridi la kawaida, ndiyo kwanza nimwombee. Mungu atamponya maskini mwanamke huyo. Yeye hakufahamu jambo hili, hakujua cho chote juu ya jambo hili. Aliingia, akasema hakujua. Lakini nilimwambia, aje anione. Alikuwa mwoga kwa namna fulani na ni mtu asiyeendelea, lakini Kiongozi aliendelea kumwambia, "Songa mbele." Akalipata. Naam. Mnaona, ni kwa sababu ya Roho Mtakatifu anayetuongoza kwenye mambo haya. Mnaona, Mungu ana njia aliyoiandaa.

72 Hivi wewe uliwahi...Umekuwa ukiona bata Bukini wa mwituni wakienda, bata wakienda kusini? Vema, sasa kumbukeni, maskini bata huyo wa kale alizaliwa huko kwenye kidimbwi mahali fulani. Yeye hajui mashariki, kaskazini, magharibi na kusini. Hajui kitu ila kile kidimbwi kilicho juu pale kwenye milima ya Canada. Yeye hajawahi kutoka kwenye kidimbwi hicho, bali yeye alizaliwa akiwa kiongozi. Maskini bata dume huyo alizaliwa awe kiongozi. Basi jambo la kwanza, usiku mmoja kulikuweko na theluji kubwa iliyokuja juu ya milima. Nini kinatukia? Hewa hiyo baridi inashuka kuvuka pale. Ninaweza kumwazia akitetemeka, akisema, "Mama, jambo hili lina maana gani?" Mnaona, yeye hajawahi kusikia hali hiyo ya hewa ya baridi bado. Anaanza kuangalia kila mahali, anaanza kuangalia kila mahali ukingoni mwa kile kidimbwi, inaanza kuganda kwa baridi, barafu ikiingia kwenye kidimbwi. Yeye hana habari, lakini mara moja...Yeye alizaliwa kuwa kiongozi wa kundi hilo la bata. Yeye atarukia aende moja kwa moja katikati ya kile kidimbwi wakati kitu hicho kinapomgusa. Kiite utakavyo. Sisi tunakiita kuvuviwa, ama waweza kukiita, loo, silika tu, cho chote kile. Yeye atarukia aende moja kwa moja katikati ya kile kidimbwi, ainue maskini mdomo wake mdogo hewani, kisha aseme, "Honk-honk, honk-honk!" Na kila bata kwenye kile kidimbwi atamjia moja kwa moja. Kwa nini? Wao wanajua kiongozi wao, jinsi tu anavyopiga makelele.

73 "Kama baragumu ikitoa sauti isiyojulikana, ni nani anayeweza kujiandaa kwa vita?" Sawa. Ni nani anayeweza kujiandaa kwa vita kama tarumbeta ikitoa sauti isiyojulikana?

74 Vema, kama maskini bata huyo akitoa sauti isiyojulikana, ni nani atakayejiandaa kwa kuruka? Maskini bata huyo wa kale atainua mdomo wake mdogo huko nje, na kupiga makelele, "Honk-honk, honk-honk!" Na kila bata mdogo atamjia. "Hon-honk, honk-honk!" Hawa hapa wanakuja. Watakuwa

na sikukuu kubwa sana, pale pale katikati ya kidimbwi, wakifingirika tu na kufingirika na kufingirika. Baada ya muda kidogo anaisikia ikisogea juu yake, hana budi kuondoka. Atatanda mbawa zake ndogo chini na kuruka kutoka kwenye hicho kidimbwi, anaruka juu hewani na kuzunguka mara nne ama tano, anaenda moja kwa moja mpaka Louisiana awezavyo kwenda, kila bata moja kwa moja nyuma yake. "Honk-honk, honk-honk," huyu hapa anakuja. Kwa nini? Yeye ni kiongozi! Amina! Bata wanajua kiongozi wao, kanisa halijui. Naam, yeye anajua la kufanya.

75 Waangalie hao maskini bata bukini, moja kwa moja kutoka Alaska. Naam, kuna maskini bata dume ambaye daima huwaongoza, nao hao bata hawana budi kumwangalia bata huyo dume vizuri sana. Hawana budi kujua anachosema huyo bata dume. Je! mlipata kusoma hilo kwenye gazeti la *Look* hapa yapata miaka minne iliyopita, ambapo maskini bata mmoja dume wakati mmoja hakujua alichokuwa anafanya, naye akawaongoza kundi la bata bukini kote kote mpaka Uingereza? Hiyo ni kweli. Hawajawahi kuonekana Uingereza hapo kabla. Kwa nini? Wao hawakumwangalia kiongozi wa— wao. Maskini bata huyo dume hakujua alikokuwa anakwenda. Basi sasa wako kule wala hawawezi kurudi.

76 Hiyo ndiyo shida ya wengi wa hawa bata bukini leo, wangali wanakusanyika. Wao wanasema, gazeti la *Look* lilisema, bata bukini hawa hukusanyika na kuruka kila mahali Uingereza, bali hawajui namna ya kurudi. Hivyo ndivyo ilivyo kwa baadhi ya hawa bata bukini ninaojua habari zao. Mna msongamano, na mkutano mkubwa wa mfululizo, kisha mnamwalika mwana ufufuo fulani aje ahubiri kwa muda kidogo, bali hamjui mnakoelekea. Mnazunguka na kuzunguka makundi makundi, kwa maana mna bata dume la bukini linalowaongoza na kuwaelekeza kwenye harakati za kimadhehebu; na si kurudi kwenye Neno la Mungu, kurudi kwenye Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Ndipo tunashangaa kwa nini hatuna ufufuo katika siku zetu. Mnaona? Hamna budi kupata Sauti hiyo inayojulikana! Sauti hiyo ni baragumu ya Injili ikipumua Injili, kila Neno la Mungu. Si kanuni ya imani, si madhehebu; bali Biblia, Roho Mtakatifu. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Mnaona? Nao hao hapo wakishuka kwenda barabarani.

77 Maskini bata bukini mmoja wakati mmoja, wao walisema, aliua kundi, akijaribu kuwarusha kupitia gizani, hakujua alikokuwa anaenda, yeye mwenyewe, ndipo wote wakagonga kwenye milima kule nje, na baadhi yao wakavunjika vipande-vipande, wakapasuka. Hakika! Hawana budi kujua sauti yao inayojulikana. Maskini bata yule wa kale, kama ana sauti dhahiri na kila mtu anaijua, wao wana sikukuu kidogo ya

kukusanyika pamoja kisha wanaenda zao kusini. Kwa nini wanaelekea kule chini? Ambako hakuna baridi.

78 Naam, kama Mungu akimpa bata akili ya kutosha kujua jinsi ya kuepa baridi, ni vipi Yeye anapaswa kulikirimia kanisa? Kama bata anaweza kufanya jambo hilo kwa silika, na Roho Mtakatifu kanisani je? Anapaswa kutuongoza kutoka kwenye taratibu za kale na kanuni za imani na kadhalika, atuingize katika ubatizo wenye utukufu na wa ajabu wa Roho Mtakatifu, ambamo mna nguvu, maarifa, saburi, utauwa, na Roho Mtakatifu. Huko ndiko Kiongozi halisi atakakoongoza, maana Yeye hatapumua kitu ila Injili, Neno la Mungu tu. Hakika, unahitaji Kiongozi!

79 Wakati, wale mamajusi, hawakujua kitu juu ya Mungu. Walikuwa—walikuwa wafanya mazingaombwe, wanajimu. Walikuwa kule mashariki. Mwajua, Biblia ilisema, "Tumeiona Nyota Yake Mashariki, tumekuja kumwabudu." Wao walikuwa wametoka magharibi, wakaangalia mashariki kisha wakaona Nyota Yake...ama wakaangalia magharibi, walikuwa Mashariki. Sisi tulikuwa Mashariki, nasi tukaiona Nyota Yake magharibi. Mnaona? "Tumeiona Nyota Yake Mashariki." Basi, unaona, wao walikuwa Mashariki. "Tulipokuwa Mashariki tuliiona Nyota, nasi tumekuja kumwabudu."

80 Ninaweza kuwazia ninawaona jamaa hao wakijiandaa kwenda. Ninaweza kuwazia mmoja wa wake zao alimwambia, kasema, "Aisee, umefungasha kila kitu, bali dira yako iko wapi?"

Akasema, "Mimi—mimi sitatumia dira wakati huu."

81 Kasema, "Utavukaje hiyo milima?" Kumbukeni, iliwabidi kuvuka Mto Tigris na kushuka wakipitia kwenye nchi tambarare, halafu, mbona, walikuwa na safari ya miaka miwili juu ya ngamia. Watafanyaje jambo hilo? Kasema, "Vema, hata hatuchukui dira."

Kasema, "La."

"Mtaendaje?"

82 "Nitaenda njia iliyoandaliwa na Mungu. Nyota ile huko ng'ambo itaniongoza kwa Mfalme yule." Haya basi.

83 "Tumeiona Nyota Yake Mashariki, kisha tukaifuata kila mahali mpaka huku magharibi, kumwabudu. Yuko wapi?" Wao waliifuata njia iliyoandaliwa na Mungu. Wao walifungwa na tita la kanuni za imani kule chini kwa muda kidogo. Wakaingia Yerusalemu na kuanza kwenda huku na huko mitaani, watu hawa waliovalia nadhifu sana, wakisema, "Yuko wapi? Yuko wapi aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi?" Vema, hayo yalikuwa ndiyo makao makuu, huo ulikuwa ni Yerusalemu. Hakika kanisa kubwa linapaswa kujua jambo fulani juu Yake. "Yuko wapi?

Yuko wapi Yeye aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi? Tumeona Nyota Yake Mashariki, tumekuja kumsujudu. Yuko wapi?"

84 Mbona, walienda kwa Mchungaji *Fulani* na kwa Kuhani Mkuu *Fulani*, hakuna mmoja wao aliyejua kitu juu ya jambo Hilo. "Mbona kuna Mtu aliyezaliwa Mfalme wa Israeli, yuko wapi?" Hawakujua.

85 Lakini kulikuwa na kundi la wachungaji huko nje kwenye mimba ya kilima wakiwa tu na wakati mzuri, naam, bwana, kwa maana wao walikuwa wamekuja katika njia iliyoandaliwa na Mungu.

86 Kwa hiyo wakakaa kule, na moja kwa moja akasema, "Nitawaambia yale tunayopaswa kufanya, tunapaswa kuwa na mkutano wa halmashauri." Kwa hiyo wao wakaita Baraza la Wazee, na—nao wakafikiria kama walisikia jambo lo lote kuhusu jambo Hilo. "La, hatukujua kitu juu ya jambo Hilo."

87 Ndivyo ilivyo leo. Hawajui kitu juu ya Kiongozi huyu, Roho Mtakatifu huyu anayeponya, anayejaza, anayeokoa, anayekuja tena. Kiongozi aliyetuambia mambo haya yote yaliyotukia, hapa tumefika barabara katikati ya mambo hayo. Mpambanuzi wa mawazo ya moyo; wao hawajui kitu juu ya jambo hilo, wao wanaliita uwezo wa kushirikiana mawazo ama cho chote kile. Hawajui waseme nini juu ya jambo Hilo.

88 Kwa hiyo, mnaona, hao mamajusi, mradi . . . Kumbukeni, wao walipoingia Yerusalemu, ile Nyota ilitoweka. Na mradi mnatafuta kanuni za imani na mtu wa kimadhehebu kuwaongoza kwa Mungu, usaidizi wa Mungu utawaacha. Lakini wakati wao walipokuwa wamechukizwa na kuchoshwa na jambo hilo, kisha wakaondoka, wakaziacha kanuni za imani na madhehebu ya Wayahudi hao, wakatoka Yerusalemu, basi ile Nyota ilitokea tena nao wakafurahi kwa furaha kuu. Wao walimwona yule Kiongozi tena! Loo, jinsi ilivyo, unaingia kwenye kanisa fulani la kale baridi na la kawaida, kisha urudi kwenye lile zuri na lililo na moto, unaona Kiongozi akiongoza, ni tofauti jinsi gani! Naam, "Tumeiona Nyota Yake Mashariki nasi tumekuja kumwabudu."

89 Yoshua aliwaambia, "Sasa ninyi lifuateni hili Sanduku, maana hamjakuwa kwenye njia hii bado." Mungu hataruhusu Sanduku hilo kwenda mahali po pote ila palipo pema. Kila mtu alilifuata, naye akaenda moja kwa moja akavuka Yordani.

90 Jambo lile lile leo, kwa Roho Mtakatifu. Naam, bwana. Jambo pekee tujualo, kama ni Roho Mtakatifu ama siye, tunaona madhihi- . . . madhihirisho Yake, madhihirisho yakilithibitisha Neno la Mungu.

91 Naam, si muda mrefu uliopita, kundi la ndugu lilikuwa na damu na mafuta, na hilo ni sawa kama wao wanataka kufanya hivyo. Mimi . . . Hilo si thibitisho kwangu mimi. Thibitisho ni Maandiko, mnaona, mradi tu linathibitisha aliyosema Mungu,

hilo ni sawa. Wao walisema, "Hii ndiyo sababu una Roho Mtakatifu, una mafuta mkononi mwako." Naam, mimi—mimi siwezi kufuata jambo hilo. Mnaona? La, siamini ya kwamba mafuta yana uhusiano wo wote na jambo hilo. Na iwapo hiyo damu ndiyo itakayoponya na kuokoa, kumetukia nini kwa ile Damu ya Yesu Kristo? Kama mafuta yale huponya, na mapigo Yake je? Mnaona? Mnaona?

92 Ningetaka Kiongozi aje, anayekuleta kwenye ile Kweli ya Neno, ndipo unajua ya kwamba umelengwa mle ndani nawe uko tayari kwa kule kuhesabu kinyumenyume. Hiyo ni kweli, ukijitayarisha kuruka. Naam, bwana. Naam, kwa sababu gani? Yule Kiongozi Ndiye anayefanya jambo hilo halisi.

93 Nina Maandiko hapa, Nilikuwa nimetoa Maandiko haya, lakini nilitaka kusoma hili. Ni II Petro, sura ya 1, aya ya 21.

> *Maana unabii haukuletwa po pote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu.*

94 Unabii ulikujaje? Si kwa mapenzi ya mwanadamu, kanuni za imani za madhehebu; bali kwa mapenzi ya Mungu, wakati watu watakatifu walipoongozwa na Roho Mtakatifu. Yeye daima amekuwa Kiongozi wa Mungu. Huyo alikuwa ni Roho Mtakatifu aliyekuwa katika Nguzo ile ya Moto, huyo alikuwa ni Roho Mtakatifu, mtu ye yote anajua huyo alikuwa ni Kristo. Musa aliacha Misri, akihesabu ya kuwa kushutumiwa kwake Kristo ni utajiri mkuu kuliko ule wa Misri. Kristo alikuwa Ndiye! Vema, wanaposimama pale na kusema, "Vema, Wewe unasema Wewe Ndiwe. Mbona, hujapata bado umri wa zaidi ya miaka hamsini, Nawe unasema umemwona Ibrahimu?"

95 Akasema, "Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO." MIMI NIKO ndiye aliyekutana na Musa katika ile Nguzo ya Moto kwenye kijiti kilichowaka moto. Naam, bwana. Yeye alikuwa Mungu aliyefanyika mwili. Si mtu wa tatu; Mtu yule yule katika afisi tofauti. Si miungu watatu; afisi tatu za Mungu mmoja. Kweli.

96 Vema, sasa, Maandiko. Daima, wakati Mungu anapotoa, anatoa yaliyo bora kuliko yote. Mungu anapoandaa njia ya kulilinda kanisa Lake, Yeye aliandaa iliyo nzuri kuliko zote. Alipompa Adamu na Hawa, katika bustani ya Edeni, kile alichowapa ni Neno Lake. "Ninyi kaeni nyuma ya Neno hili, nanyi mko salama. Lakini, kama mkiondoka Kwake, siku mtakayokula hayo siku hiyo mtakufa." Mungu hajabadilisha mbinu Zake. Wala Shetani hajabadilisha zake; jinsi alivyoingia ndani ya Adamu na Hawa, anawaingia leo. Kwa nini? Kwa kujaribu kulihoji Hilo. "Naam, ni kweli kwamba Mungu hangefanya hivyo. Loo, Mungu amesema," kasema Shetani, "lakini hakika Mungu mtakatifu asingefanya jambo hili." Bila shaka atafanya, kwa maana Yeye alisema angefanya!

97 Na jambo hilo ndilo watu wanalosema leo, “Loo, sasa ngojeni! Hamwamini sasa, kama nikienda kanisani na kulipa fungu langu la kumi, na kufanya jambo *hili*, na lile *lingine*, Mungu atanitupa?” Mtu asipozaliwa mara ya pili, yeye hata hataufahamu Ufalme wa Mungu! Mnaona? Hamna udhuru! “Vema, maskini yule mzee, maskini mwanamke yule mzee, huyo hapo mtu mzuri.” Jinsi tu wanavyoweza kumwona Mungu, ni kuzaliwa mara ya pili. Hivyo tu. Sijali ni wadogo namna gani, wana umri mkubwa namna gani, wana umri mdogo namna gani, walilofanya, mara ngapi walikwenda kanisani, wanajua madhehebu mangapi, wanaweza kukariri kanuni ngapi za imani. Huna budi kuzaliwa mara ya pili la sivyo hata huko juu ya msingi, kwanza. Hiyo ni kweli kabisa.

98 Kwa hiyo, unaona, unahitaji Kiongozi. Atakuongoza kwenye Kweli, nayo Kweli ni Neno. Atakuongoza. Na daima imekuwa hivyo. Haimlazimu Mungu kubadilisha cho chote, maana Yeye hana kikomo naye anajua yaliyo bora kuliko yote. Yeye yupo kila mahali, anajua yote, Yeye—Yeye ni kila kitu. Ni kweli, Mungu ni hayo, kwa hiyo si lazima abadilike. Vema.

99 Yeye ni Mthibitishaji wa vile anavyokuongoza. Roho Mtakatifu, yule Kiongozi, ni Mthibitishaji wa Neno lile lile ambalo anafundisha. Naam, Luka aliongozwa na yule Kiongozi, kusema, “Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokolewa, asiyeamini atahukumiwa. Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; katika Jina Langu watatoa pepo, watanena kwa lugha mpya, watashika nyoka, watakunywa vitu vya kufisha, wataweka mikono juu ya wagonjwa nao watapata afya.” Nayo Biblia ilisema ya kwamba, “Walienda kila mahali,” wakiongozwa na Kiongozi, mwajua, “wakahubiri Neno, na ishara zikifuata.” Ilikuwa ni nini? Kiongozi akithibitisha Hayo yalikuwa ni Kweli!

100 Hiyo ilikuwa ndiyo kanuni ya Mungu. Hivyo ndivyo ilivyoamriwa. Huo ndio mpango Wake; hawezi kuubadilisha, kwa sababu Yeye hana kikomo. Amina. Hawezi kuubadilisha; Yeye ni Mungu. Ninaweza kubadilika; mimi ni mwanadamu. Unaweza kubadilika; wewe ni mwanamume ama ni mwanamke. Bali Mungu hawezi kubadilika. Mimi nina kikomo; ninaweza kufanya kosa na kusema mambo vibaya, sisi sote tunaweza. Bali Mungu hawezi, na awe Mungu. Uamuzi Wake wa kwanza ni mkamilifu. Jinsi Mungu anavyotenda hadharani, hivyo ndivyo jinsi ambavyo hana budi kutenda kila wakati. Kama akiitwa hadharani kumwokoa mwenye dhambi, Yeye anamwokoa kwa msingi wa jambo moja. Mara nyingine mwenye dhambi akija tena, Yeye hana budi kutenda vile vile, la sivyo alikosea alipotenda mara ya kwanza. Amina. Ninampenda. Ninajua ni Kweli.

101 Mimi nina umri wa miaka hamsini na mitatu, nimekuwa nikihubiri Injili hapa kwa miaka thelathini na mitatu u nusu,

sijapata kuona Hiyo ikishindwa. Nimeiona ikijaribiwa mara saba kote ulimwenguni, katika dini za kila namna na cho chote kile, mbele ya watu wapatao nusu milioni wakati mmoja, wala haijashindwa kamwe. Mimi sizungumzi kutoka kwenye kitabu fulani, ninazungumza kutokana na ujuzi wa kibinafsi, kwamba ninajua ya kwamba Mungu husimama nyuma ya Neno Lake na kuliheshimu. Naam, kama una namna fulani ya kanuni za imani, afadhali uangalie jambo hilo. Lakini Roho Mtakatifu atalishindania Neno la Mungu.

102 Katika Yohana Mt., sura ya 1 na aya ya 1, yeye alisema, "Yeye ni Neno. Yeye ni Kiongozi. Hapo mwanzo kulikuweko Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili akakaa kwetu." Jamani!

103 Petro aliongozwa kusema, kwenye Matendo 2:38, jinsi ya kumpokea Roho Mtakatifu, akasema, "Tubuni, kila mmoja wenu, halafu mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, halafu Kiongozi atawachukua kutoka hapo na kuendelea." Naam, hilo ndilo jambo la kufanya. Kwanza, tubuni dhambi zenu, kutokuamini kwenu, kwamba hamkuyaamini mambo haya. Tubuni, halafu mbatizwe, ndipo yule Kiongozi atawachukua kutoka mahali hapo na kuendelea. Mnaona, huo ndio wajibu wenu. Ni wajibu wenu kutubu. Ni wajibu wenu kubatizwa. Halafu ni wajibu wa huyo Kiongozi kuwachukua kutoka mahali hapo na kuendelea, kuwaongoza kutoka kwenye wema hadi kwenye maarifa, kwenye kiasi, kwenye saburi, kwenye utauwa, na kwenye upendano wa ndugu, naye Roho Mtakatifu anakutia muhuri. Mnaona? Ndipo wewe ni kiwango kikamilifu cha Mungu, mwanamume halisi wa Mungu, mwanamke halisi wa Mungu, umetiwa nanga katika Kristo. Ninapenda jambo hilo, huko kutiwa nanga katika Kristo.

104 Naam, Marko aliongozwa na Roho Mtakatifu, kuandika Marko 16, bila shaka.

105 Yohana aliongozwa alipoandika Ufunuo. Yeye aliongozwa na Kiongozi. Pia aliongozwa na Kiongozi kusema, "Yeye atakayeondoa Neno moja kutoka Kwake, ama kuongeza neno moja Kwake, yeye ataondolewa, sehemu yake, kutoka katika Kitabu cha Uzima."

106 Naam, utabadilishaje kitu fulani kwa Neno la Mungu, na bado useme unaongozwa na Roho Mtakatifu? Halina maana, sivyo? La, bwana. Halina.

107 Yeye amekuwa Kiongozi wangu maishani mwote. Yeye ameniongoza maishani. Yeye ndiye aliyeniongoza Maishani, Naye ndiye Maisha yangu. Bila Yeye mimi sina Uzima. Bila Yeye mimi sitaki kitu kingine. Yeye ni Yote-katika-Yote kwangu. Katika saa za shida zangu, Yeye husimama karibu nami. Jana alinibariki, leo wamefanya vile vile. Ninaweza kutarajia nini? Jambo lile lile milele, Jina Lake lisifiwe! Amina? Naam, bwana.

Yeye aliahidi jambo hilo. Atalitekeleza. Yeye ndiye Uhai wangu, Yeye ndiye Kiongozi wangu, ni Yote-katika-Yote. Nimemwamini Yeye. Nimekuwa na majaribu magumu. Ninamtumaini po pote niendapo. Ninataka ninyi mfanye jambo hilo. Kama mkienda kufua nguo, enyi wanawake, mtumainini Yeye. Kama mkienda mjini, mtumainini Yeye.

108 Ilifikia wakati mmoja ambapo nilifikiri kwamba mimi nilikuwa kwa namna fulani ni mtu hodari wa mwituni, unajua, nimewinda sana. Nikafikiri, "Mimi hakika sidanganyiki, hakuna mtu atakaye-. . . Usingeweza kunipoteza. Mama yangu alikuwa nusu Mhindi, nami nilipenda jambo hilo. Loo, jamani! Huwezi kunipoteza mwituni, mimi ninajua mahali nilipo."

109 Nami huyo. . . fungate yangu, kwa namna fulani nilimhadaaa mke wangu, nikamwambia, "Wajua, mpenzi, lingekuwa ni jambo zuri kwetu kufunga ndoa Octoba ishirini na tatu." Bila shaka, hiyo ndiyo siku Bwana aliniambia nifanye jambo hilo.

110 Nami nikawazia, "Naam, laiti ningepata fungate ndogo! Niliweka pesa zangu, nami nitampeleka karibu na Maporomoko ya Niagara, kisha tupande milima Adirondack na kuwinda kidogo." Unaona? Kwa hiyo nikamchukua yeye pamoja na Billy, yeye alikuwa ni kitoto kidogo tu. Na kwa hiyo ilinibidi kumpeleka kwenye fungate, nayo ilikuwa safari ya kuwinda, pia, mwajua. Kwa hiyo—kwa hiyo nilifikiri jambo hilo lingekuwa jema kufanya. Basi nikakwea naye, na . . .

111 Nikamwandikia Bw. Denton, yule mlinzi. Nasi tulikuwa tukienda kweye Mlima wa Hurricane. Basi nikasema, "Bw. Denton, ninakuja, ninataka kuwinda dubu pamoja nawe kwenye msimu huu wa mwisho wa mwaka."

112 Naye akasema, "Sawa, Billy, kwea uje." Kwa hiyo akasema, "Nitakuwa kule juu kwenye tarehe fulani." Vema, mimi na mke wangu tulifika kule siku moja mapema, na Billy, na kwa hiyo kile kibanda kilikuwa kimefungwa, na kulikuwako na mahali pa kujiegemeza kule mwituni.

113 Ambako, mimi pamoja na Ndugu Fred Sothmann tulienda si muda mrefu uliopita na kusimama pale. Roho Mtakatifu, nilimwona amesimama pale, hiyo Nuru ya manjano ikizunguka kichakani, naye Fred amesimama papo hapo. Akasema, "Njoo huku kando, nataka kuzungumza nawe. Kesho," kasema, "uwe mwangalifu, wamekuwekea mtego." Kasema, "Uwe macho!" Hiyo ni kweli, Ndugu Fred? Nami nikaondoka na kuwaambia mamia ya watu usiku huo, kule Vermont, nikasema, "Kuna mtego nimetegewa; nitauona. Sijui uko wapi." Basi usiku ule ule uliofuatia, huo hapo unakuja, huo hapo. Kasema, "Huu hapa mtego ambao ulitegwa." Naam, bwana. Lakini Roho Mtakatifu aliniongoza katika jambo la kufanya. Na, loo, jamani, hiyo

ilikuwa kweli kabisa! Loo, wengi wenu mnajua ulikuwa ni nini. Sina wakati wa kusimulia jambo hilo.

114 Lakini nikiwa nimesimama mahali pale wakati huo, kukaanza tu kugeuka kuwa na baridi siku hiyo. Bw. Denton alikuwa yuaja kesho yake, nikasema, "Wajua, mpenzi, lingekuwa ni jambo jema kama ningelipata du—dume mkubwa wa kulungu wa kumpeleka nyumbani." Nikasema, "Tulinini hii . . . Ilinibidi kuhifadhi hela hizi, nasi ndiyo kwanza tufunge ndoa." Nami nikasema, "Tungepata nyama yetu ya kipupwe kama ningewinda kidogo leo."

115 Basi akasema, "Vema, endelea, Billy." Kasema, "Sasa, ukumbuke, mimi kamwe sijapata kuwa kwenye misitu hii," akasema. Alikuwa kama maili ishirini na tano juu milimani, mwajua, naye akasema, "Sijui lo lote juu ya jambo hili."

116 Naye akasema, kwa hiyo mimi . . . Nami nikasema, "Vema, sasa, mnakumbuka, ilikuwa miaka miwili iliyopita nilipowaua wale dubu watatu. Hiyo ilikuwa moja kwa moja huko juu ya mlima ule pale." Basi nikasema, "Naam, nitapata dume mkubwa wa kulungu nasi tutapata dubu," kisha nikasema, "tutapata nyama yetu ya kipupwe." Vema, hilo lilisikika zuri sana, mwajua. (Nasi tukachuma forsadi, na kupata makaa yetu kwa hicho—kwa ajili ya kipupwe hicho; na kwa hiyo basi Billy akaziuza, nami na Meda tukazichuma jioni moja baada ya mimi kutoka kwenye doria yangu.) Kwa hiyo basi ni— nikasema, "Vema, nitaenda nichukue bunduki yangu, nitashuka niende huku chini." Nikasema, "Kuna kulungu wengi sana humu ndani, nitampata mmoja." Nami nikasema, "Unajua," nikasema, "basi nitampata." Ndipo nikasema, "Vema . . . nitarudi katika muda mfupi."

Akasema, "Sawa."

117 Kwa hiyo, nilipoanza kwenda, kwa namna fulani baridi ilikuwa imeanza. Basi ye yote wenu watu wa New Hempshire, na juu huko New England, mnajua inamaanisha nini wakati ukungu huo unaposhuka, ama po pote pale milimani, hujui uko wapi. Hivyo tu. Huwezi kuona mkono wako mbele yako. Kwa hiyo nikashuka nikaenda kupitia kwenye mwanya m—mdogo, kitu kama hicho, nikashuka, ndipo nikaenda upande wa pili wa ule mwinuko mdogo na kupanda juu. Nami nikamwona chui, ndivyo mngemwita hapa katika sehemu hii ya nchi. Sisi tunamwita, huko Magharibi, koga. Wao wanamwita, kule juu, simba wa milimani. Ni mnyama yule yule. Ni puma, ndivyo alivyo hasa. Paka yule yule, mwenye urefu wa kama futi tisa, naye ana uzito wa kama ratili mia moja hamsini, mia mbili. Akavuka barabara, nami nikatoa bunduki haraka sana, si haraka vya kutosha kumpiga risasi.

118 Vema, nikakimbia juu ya kile kilima, nikimfukuza koga huyu, nikiangalia majani alikopitia, mwajua. Niliweza

kumsikia. Alikuwa na miguu minne. Nilijua hakuwa mnyama mwenye miguu miwili, miguu yake minne. Nami nilijua hakuwa kulungu, maana kulungu hufanya vishindo kwa miguu. Naye angeponyoka kwa urahisi sana, yule paka, wajua, namna hiyo. Naye dubu hufingirisha miguu yake anapotembea. Na kwa hiyo nilijua hapana budi ni koga. Naye alikuwa nyuma ya gogo nami sikumwona, hata nilipopata kumwona kidogo tu, amekwisha kwenda.

119 Basi nikaangalia jinsi alivyoyavuruga majani, unajua, huko juu ya mlima, na kushuka chini namna hii, nami sikuwa nikiangalia lile wingu linalokuja wakati wote ule, mwajua, ule ukungu ukishuka. Nikashuka upesi, nikapitia kwenye bonde kubwa kisha nikashuka nikaingia kwenye miti mikubwa mno, nikimfuatilia koga huyu. Nikawaza, "Nitampata baada ya kitambo kidogo." Ningeona mahali fulani, nami ningekimbia nikapanda mahali palipoinuka, na kuangalia kila mahali namna hiyo, na kuchungulia kila mahali, nione kama ningeweza kumwona; ningesikiliza kwa makini sana, kisha ningeshuka, ningeshuka haraka tena. Ungeweza kusikia majani madogo yakigongana, mbele yake kabisa alipokuwa anatoka. Mnaona, alikuwa akigongagonga miti wakati huo kwamba sikuweza kumfuatilia. Mnaona, akawa mwerevu, akapanda kwenye miti na alikuwa akiruka kutoka kwenye mti mmoja hadi mwingine. Basi alijua nisingeweza kumfuatilia kule. Loo, nikawaza, "Loo, haidhuru!"

120 Basi nikaanza kupanda yale magenge, ndipo nikanusa harufu ya dubu, dubu mzee dume. Nikawaza, "Nitampata sasa, aisee, hilo ni sawa!" Nikanusa harufu tena, ndipo nikaenda mbele kidogo, nami nikaangalia kila namna za ishara na kila kitu. Sikuweza kuona kitu; nikageuka nirudi chini, kisha nikashuka nikarudi upande wa pili wa ule mlima. Ndipo nikaanza kuona, kidogo kuna hali ya ukungu-ukungu inaingia. Nami ningenusa ile harufu tena, alikuwa hewani mahali fulani. Nikasema, "La. Sasa, jambo lililotukia, upepo ulikuwa unakuja namna *hii*, nami nikanusa harufu ya yule dubu ikija kutoka upande huu chini *kule*, nami nimevuka hapa sasa nao upepo unatokea upande huu mwingine. Kwa hiyo inanibidi kurudi mahali niliponusia harufu ya yule dubu mara ya kwanza, na kuichukua kuanzia hapo."

121 Basi nilipokuwa ninarudi, niliangalia upande wa pili wa yale magenge, nikaona vile vichaka vikisogea. Ndipo nilipofanya hivyo, kitu cheusi kikasogea. Nikawaza, "Huyo hapo." Nikaingiza risasi katika bunduki, upesi sana, kisha nikasimama kimya. Basi, aliposogea, ilikuwa ni dume mkubwa mno wa kulungu, mkubwa mno. Nikawaza, "Huyu ndiye niliyekuwa nikitaka hasa, kwa vyo vyote." Nikamuua kwa risasi yule kulungu.

122 Nikawaza, “Vema!” Sikuona ilikuwa kwa namna fulani... Mnamo wakati nilipomaliza kumtengeneza, nikaangalia... Nikasafisha mikono yangu na kutayarisha kisu changu, nikakirudisha. Ndipo nikawaza, “Mungu asifiwe! Asante, Bwana Yesu, umenipa nyama yangu ya kipupwe. Mungu asifiwe!” Ndipo nikachukua bunduki yangu. Nikawaza, “Nitarudi moja kwa moja kule juu ya magenge haya sasa.” Nikasema, “Angalia hapa, kijana, dhoruba inakuja. Afadhali nitoke hapa nirudi kule aliko Meda na hao wengine.” Nikasema, “Sina budi kuharakisha.”

123 Nikapanda magenge haraka, nikafungua kabuti langu kubwa jekundu, nami nilikuwa ninakimbia nikielekea juu ya magenge namna hii, ninazunguka. Muda si muda, nikawaza, “Jamani, hivi niligeukia wapi?” Upepo tayari ulikuwa umeshuka, miti ikigongana. Nikawaza, “Hivi niligeukia wapi?” Nikazunguka. Ni—nilijua nilikuwa nikienda moja kwa moja kwenye Mlima wa Hurricane. Lakini ikawa kwamba nilisimama, nami nilikuwa ninatokwa na jasho, nikawaza, “Kuna nini hapa? Nimekwenda kwa nusu saa, ama theluthi tatu, nami siwezi kuona mahali nilipogeukia.” Nikaangalia juu, huyo hapo kulungu wangu amening’inia. Nilikuwa mahali pale pale. Nikawaza, “Vema, nilifanya nini?”

124 Vema, nikaondoka tena. Nikawaza, “Nitafaulu safari hii, sikuwa kabisa ninaangalia.” Niliangalia kila hatua ndogo kila mahali, nikiangalia. Nikaendelea kutafuta, kutafuta, kutafuta. Hayo mawingu yakija, nilijua dhoruba ilikuwa yaja, huku ukungu umeshuka chini, halafu nikaanza kuona. Nikawaza, “Nitaenda mbele kidogo,” nikazidi kwenda, na kwenda, na kwenda, na kwenda, na kwenda, na kwenda, na kwenda. Basi nikawaza, “Vema, ajabu hii, inaonekana kana kwamba nimekwisha paona mahali hapa hapo kabla.” Basi nikaangalia, huyo hapo kulungu wangu amening’inia pale. Mnaona?

125 Mnajua nilikuwa kwenye nini? Wahindi wanauita “mwendo wa mauti.” Unaona, unatembea katika duara, unazunguka na kuzunguka. Vema, nilifikiri nilikuwa kiongozi mzuri sana nisingeweza kupotea. Mnaona, hakuna kitu kilipaswa kunieleza habari za mwituni, nilijua kila mahali. Unaona?

126 Ndipo nikaanza tena. Nikasema, “Siwezi kufanya kosa hili.” Ndipo nikarudi tena.

127 Nilipanda yale magenge umbali mdogo kidogo, halafu upepo ulikuwa umeanza kuvuma. Loo, jamani, theluji kila mahali! Ilikuwa kabisa inaelekea usiku. Nami nilijua ya kwamba Meda angekufa usiku huo porini, hakujua jinsi ya kujishughulikia. Naye Billy alikuwa tu na yapata umri wa miaka minne, umri wa miaka mitatu, kijitoto kichanga tu. Basi nikawaza, “Watafanya nini?” Vema, nilipanda umbali huu ndipo nikafika mahali penye sehemu tambarare yenye ukungu mdogo, nikawaza, “Niko

mahali fulani tambarare, nami siwezi kuona kitu, pamejaa ukungu." Nilikuwa ninazunguka sasa.

128 Kwa kawaida, ningalijitafutia mahali na kushikilia, kama ningalikuwa pamoja na mtu fulani. Ningeshikilia na kungoja mpaka dhoruba imekwisha, siku moja ama mbili, kisha nitoke. Nikate kipande changu cha kulungu. . .nikiweke mgongoni mwangu, na niingie, nile, na nisahau jambo hilo. Bali huwezi kufanya jambo hilo, huku mke wako na mtoto mchanga wako kule mwituni, wakiangamia. Mnaona?

129 Kwa hiyo nikaanza kufikiri, "Nifanye nini?" Kwa hiyo nikasonga mbele kidogo. Basi nikawaza, "Sasa, ngoja. Nilipovuka lile bonde la kwanza, upepo ulikuwa unanipiga usoni, kwa hiyo sina budi nilitokea kwa upande huu. Sina budi kuja namna hii." Nami nilikuwa nimetangatanga huko chini kabisa kwenye ile miti mirefu sana, bali sikujua nilikokuwa. Nikasema, "Loo!" nikaanza kushikwa na wasiwasi. Ndipo nikawaza, "Ngoja kidogo, Bill, hujapotea," nikijaribu kujidanganya. Huwezi kujidanganya. La, la. Dhamiri ile ya ndani inakwambia umekosea.

130 Loo, u—unajaribu kusema, "Loo, mimi nimeokoka, ninaenda kanisani." Usijali, wewe ngoja mpaka mauti yakaribie, nawe utajua ni tofauti. Dhamiri yako inakwambia. Kitu fulani ndani yako kinakwambia umekosea. Mnaona? Unajua kama ukifa usingeweza kukutana na Mungu mtakatifu. Kama tulivyomwona jana usiku, hata Malaika watakatifu hawana budi kufunika uso wao wapate kusimama mbele Zake. Wewe utasimamaje bila ya kufunikwa na Damu ya Yesu Kristo?

131 Nikawaza, "Loo, nitafaulu." Nikaanza kwenda. Ndipo nikapata kutambua kwamba nilikuwa naendelea kusikia Kitu Fulani. Ndipo nikashikwa na wasiwasi. Nami nikawaza, "Sasa, kama nikifanya hivyo, nitachanganyikiwa." Kwa kawaida hivyo ndivyo anavyofanya mtu aliyepotea, yeye atachanganyikiwa huko mwituni. Basi atachukua bunduki yake, anajiua; ama aanguke kwenye handaki na kuvunja mguu wake, ndipo hapo atakaa, atafia pale. Kwa hiyo nikawaza, "Nitafanya nini?" Kwa hiyo nikaanza kusonga mbele.

132 Basi nikaendelea kusikia Kitu Fulani kikisema, "Mimi ni msaada upatikanao wakati wa shida." Nami nikaendelea tu kutembea.

133 Nikawaza, "Naam, ninajua ninachanganyikiwa kidogo sasa, ninasikia sauti ikinena nami." Nikaendelea kusonga mbele. Upepo nao, "whi, whi, whi," unavuma, mwajua. Nikawaza, "Sasa, sijapotea. Unajua ulipo, kijana! Una shida gani? Huwezi kupotea. Wewe—wewe ni mwindaji bora sana, huwezi kupotea." Nikijisifu mwenyewe, unajua, nikijidanganya mwenyewe kabisa.

134 Huwezi kujidanganya. *Huku* chini kabisa kuna gurudumu dogo linalozunguka, likisema, "Kijana, umepotea nawe unajua umepotea. Unaona, umepotea."

135 Nikaendelea kusonga mbele. "Loo, sijapotea! Nitakuwa sawa. Nitapata njia yangu ya kutokea." Mambo yakaanza kubadilika, upepo ukakaribia. Theluji ikaanza kuruka, ile theulji ndogo kama unga, tunaiita "inayotema chini." Ndipo niliwazia habari za mke wangu na mtoto mchanga. Mimi si-. . . Nikawaza, "Loo, jamani!"

136 Mara nikasikia jambo Hilo tena, kasema, "Mimi ni Msaada upatikanao wakati wa shida." Nami nilikuwa mhudumu wa Injili wakati huo, nikihubiri papa hapa maskanini.

137 Kwa hiyo nikawaza, "Vema, nifanye nini?" Nikasimama, nikaangalia kila mahali, na ukungu ulikuwa umeshuka sasa. Mimi . . . Haya basi. Hakuna kitu kingeweza kufanyika wakati huo. Nikawaza, "Loo, nifanye nini?" Nikawaza, "Bwana, mimi sistahili kuishi, nimejitumaini kupita kiasi. Nilifikiri nilikuwa mwindaji, bali si mwindaji. "

138 Na, ndugu, daima nimemtumaini. Kupiga bunduki, nina rekodi kule. Na mvuvi, mimi ni mbaya sana, bali daima nimemtumaini Yeye. Kupiga bunduki, mimi sijui kulenga, bali ameniruhusu nivunje rekodi za ulimwengu kwa hiyo. Mnaona? Kupiga kulungu risasi, umbali wa yadi mia saba, mia nane. Nina bunduki pale iliyowaua wanyama thelathini na watano bila kukosa risasi nayo. Soma tu jambo hilo mahali po pote, ukiweza. Unaona? Si mimi, ni Yeye. Nimemtumaini.

Mimi hapo, nikawaza, "Nifanye nini? Nifanye nini?"

139 Nikazidi . . . Hiyo ikizidi kukaribia, karibu zaidi, "Mimi ni Msaada upatikanao wakati wa shida, Msaada upatikanao."

140 Nikawaza, "Hivi huyo anayenena nami ni Mungu?" Nikatoa kofia yangu. Nilikuwa nimevaa kofia yangu ya doria, iliyozungushiwa kitambaa chekundu. Nikaiweka chini. Nikatoa koti langu, lilikuwa limelowa maji. Basi nikaweka koti langu chini, nikaegemeza bunduki yangu mtini. Nikasema, "Baba wa Mbinguni, sasa ninaanza kuchanganyikiwa, ninasikia sauti ikinena nami. Huyo ni Wewe?" Nikasema, "Bwana, nitakiri Kwako ya kwamba mimi si mwindaji. Mimi si mwindaji, si—siwezi kupata njia yangu ya kutokea. Huna budi kunisaidia. Mimi sistahili kuishi, na kufanya mambo ambayo nimefanya, kuingia hapa na kufikiri nilijua mengi sana kuhusu jambo hilo hata nisingeweza kupotea. Ninakuhitaji Wewe, Bwana. Mke wangu ni mwanamke mzuri. Mtoto wangu mchanga, mvulana wangu mdogo, mama yake amekwisha aga dunia, naye anajaribu kumlea kama mamaye, nami ndiyo kwanza nimuoe. Na yupo hapa, mtoto mchanga, kule mwituni, wote wawili watakufa usiku wa leo. Upepo huo, joto litashuka chini kama nyuzi joto kumi chini ya sifuri, nao hawatajua jinsi ya kuishi.

Watakufa usiku wa leo. Usiwaache wafe, Mungu. Nipeleke kwao, ili kwamba niweze kuona kwamba hawatakufa. Nimepotea! Nimepotea, Mungu! Si—siwezi kupata njia yangu ya kutokea. Tafadhali nisaidie? Pia nisamehe kwa ajili ya mwendo wangu mwenyewe wa ubinafsi! Siwezi kutenda kitu cho chote bila Wewe, Wewe ndiwe Kiongozi wangu. Nisaidie, Bwana."

141 Nikaamka, nikasema, "Amina." Nikachukua kitambaa changu; koti langu, nikalichukua; nikavaa kofia yangu tena; nikachukua bunduki yangu. Nikasema, "Sasa nitajiandaa niende vizuri nijuavyo kwenda, nijuavyo mimi; nami nitaenda moja kwa moja upande mmoja, maana ninatembea nikizunguka-zunguka kwenye duara mahali fulani, sijui ni wapi. Bali nitaenda jinsi unavyoniambia, Bwana Mungu, Kiongozi wangu."

142 Nikaanza kwenda *hivi*. Nikasema, "Hii ndiyo, nami sina budi kujifanya niamini jambo hilo. Ninaelekea upande *huu*. Ninaenda moja kwa moja upande *huu*. Sitabadili, ninaelekea upande *huu*. Ninajua niko sawa. Nitaelekea upande *huu*." Kama ningalienda upande ule, ningalielekea Canada. Mnaona?

143 Punde kidogo tu nikasikia Kitu Fulani kikinigusa begani mwangu, mkono, uliosikika kama mkono wa mwanadamu, upesi sana hata nikageuka kuangalia. Hapukuwepo na mtu aliyesimama pale. Nikawaza, "Hicho kilikuwa ni nini?" Hii hapa Biblia imewekwa hapa mbele yangu. Mungu, Kiongozi wangu na Hakimu wangu, anasimama hapa. Nikaangalia tu juu. Na moja kwa moja upande *huu*, ukungu huo ndiyo kwanza urudi nyuma hata niliweza kuona ule mnara kwenye Mlima Hurricane. Nikienda moja kwa moja mbali nao, kulingana na uwezo wangu wote wa kuwinda, nilikuwa nikienda mbali nao, kukizidi kuchwa kabisa jioni wakati huo. Nikageuka upesi sana, nikijiongoza namna *hii*. Nikashika kofia yangu nikainua mikono yangu, nikasema, "Niongoze, Mungu, Wewe ndiwe Kiongozi wangu."

144 Nikaanza. Ilinibidi kwenda moja kwa moja juu ya magenge na kila kitu kufika mahali pale, huku kunazidi kuwa usiku. Ndipo giza likaingia. Kulungu walikuwa wanaruka mbele yangu, na kila kitu. Nisingefikiri juu ya jambo lo lote ila kujishikilia upande mmoja, moja kwa moja kupanda mlima huu.

145 Nami najua kama ningeweza kufika kwenye ule mnara, mimi . . . mimi na Bw. Denton tulisaidia kuweka zile nyaya za simu kwenye msimu huo wa kuchanua majani. Tuliweka hizo nyaya za simu kutoka Mlima Hurricane, moja kwa moja mpaka kule chini kama maili tatu u nusu ama maili nne, moja kwa moja hadi kwenye kambi. Nayo ilitelemkia kwenye mkondo mdogo, lakini, theluji ikiwa kule juu, usingeweza kuuona ule mkondo. Unaona? Huku upepo unavuma na kila kitu, kulikuwa giza na upepo mkali wa theluji na, unavuma, usingeweza kujua

ulipokuwa. Naam, jambo pekee nililojua la kufanya, baada ya kuwa giza, nami sikujua. . . Ninajua nilikuwa nikielekea upande mmoja, na moja kwa moja kupandisha mlimani. Maana nilipaswa kupanda mlima, na ule mnara ulikaa moja kwa moja juu ya ule mlima, nami nilikuwa na kama maili sita kuufikia. Hebu wazia tu, ukungu ule ulipoondoka, maili sita, shimo moja tu, hata ningeweza kuuona!

146 Halafu mimi—ningebeba bunduki yangu kwenye mkono *huu*, na niuinue mkono *huu* juu, maana nimeupigilia misumari ule—ule waya kwenye miti namna hiyo ukishuka chini, zile nyaya za simu zinazoelekea kwenye kile kibanda, ili apate kuzungumza na mkewe, kisha apige simu kutoka hapo, kutoka mlimani. Nami nilikuwa ninaenda kumsaidia kuitoa mwishoni mwa mwaka huo. Basi nilikuwa nimeinua mkono wangu namna *hii*, nikisema, "Ee Mungu, nijalie niuguse waya huo." Nikatembea, nao mkono wangu ungeuma sana, ungechoka, ilikuwa vigumu kwangu kuushikilia, nami ingenibidi kuuweka chini. Kisha ningebadilisha ile bunduki na kuiweka kwenye *huo*; nirudi nyuma hatua chache ili kwamba niwe na hakika sitaukosa, kisha niuinue mkono wangu juu, nianze kutembea, kutembea. Kulikuwa kunazidi kuchwa, giza, upepo unavuma. Loo, ningeshika tawi upesi, ningesema, "Ndio huo! La, sio huo." Loo, hiyo inatoa . . . Usiiache itoe sauti isiyojulikana.

147 Baada ya kitambo kidogo, nilipokuwa tayari tu kukata tamaa, mkono wangu ukagusa kitu fulani. Loo, jamani! Nimekwisha patikana, nilipokuwa nimepotea. Nikashikilia waya huo. Nikaangusha ile bunduki moja kwa moja chini, nikatoa kofia yangu kichwani mwangu, nami nikasimama pale. Nikasema, "Ee Mungu, ni kujisikia kwa namna gani kupatikana, unapopotea." Nikasema, "Moja kwa moja hadi mwishoni mwa waya huu, sitauachilia kamwe. Nitaushikilia waya huu. Utaniongoza moja kwa moja hata mahali waliko wote ninaowapenda sana hapa duniani, moja kwa moja kule. Mke wangu na mtoto mchanga, wameshikwa na wasiwasi sana, hawajui niliko, hawajui jinsi ya kuwasha moto, hawajui la kufanya, huku pepo zinavuma, na matawi yakirushwa-rushwa na kuanguka kutoka mitini." Nisingethubutu kuachilia waya huo. Niliushikilia waya huo hata ukaniongoza moja kwa moja walikokuwa wote niliowapenda sana duniani.

148 Hilo lilikuwa ni tukio la kutisha, na tukio kubwa kwangu kuona njia ya kutokea, bali hilo halikuwa nusu yake. Siku moja nilikuwa nimepotea dhambini. Nilihudhuria kanisa baada ya kanisa, nikijaribu kupata Kitu Fulani. Nilienda kwa Wasabato, wakaniambia, "Shika Sabato, acha kula nyama." Nikaenda kwenye kanisa la Kibatisti, kanisa la kwanza la Kibatisti, akasema, "Simama tu uwaambie ya kwamba unamwamini Yesu Kristo Mwana wa Mungu," nami nitakubatiza, hivyo tu. Hapakuwepo na kitu. Lakini siku

moja, huko nje kwenye kibanda kidogo cha makaa, niliinua mikono yangu juu, nikashika Kitu Fulani; ama, hebu niseme, Kitu Fulani kilinishika. Ilikuwa ni ile Kamba ya Uhai, yule Kiongozi. Naye ameniongoza salama umbali huu, sitaondoa mkono wangu kwenye waya huo. Ninamwinulia Yeye mikono yangu. Hebu kanuni za imani, madhehebu yafanye lo lote yatakalo, mimi ninajishikilia kwa yule Kiongozi. Kwa yote yaliyopata kuwa duniani na yote yaliyoko Mbinguni, yote yaliyo ya thamani kwangu, yako kwenye mwisho wa waya huu. Yeye amenileta umbali huu salama, nitamtumainia kwingine kote. "Atakapokuja Roho Mtakatifu, atawaongoza na kuwaelekeza kwenye nini hii yote. . . . ."

149 Enyi marafiki, Huyo amenileta moja kwa moja nilipo leo. Amenifanya nilivyo mimi. Ninaweza kumjulisha kwenu kwa furaha. Ndiye Kiongozi pekee ninayejua habari zake, kwa hapa duniani ama huko Juu. Yeye ndiye Kiongozi wangu ninapokwenda kuwinda. Yeye ndiye Kiongozi wangu nipokwenda kuvua samaki. Yeye ndiye Kiongozi wangu ninapozungumza na mtu fulani. Yeye ndiye Kiongozi wangu ninapohubiri. Yeye ndiye Kiongozi wangu ninapolala.

150 Na ninapofikia kufa, Yeye atakuwa amesimama pale mtoni, ataniongoza nivuke. Sitaogopa mabaya, kwa maana Wewe u pamoja nami. Gongo Lako na fimbo Yako, vitanirudi na kuniongoza nivuke ule mto. Na tuombe.

151 Baba wa Mbinguni, ninashukuru sana kwa ajili ya yule kiongozi, Yule Ambaye ananiongoza mimi. Loo, wakati mwingine, Baba, siwezi kumsikia karibu nami, ninaogopa. Ninamtaka awe karibu nami kwa maana sijui ni wakati gani nitakapokimbilia mtoni. Ninamtaka awe karibu nami. Usiniache kamwe, Bwana. Siwezi kuzungumza, siwezi kuhubiri, siwezi kuwinda mwituni, siwezi kuvua samaki ukingoni, siwezi kuendesha motokaa yangu, hakuna jambo ninaloweza kufanya bila Wewe. Wewe ndiwe Kiongozi wangu. Jinsi nilivyo na furaha kuliambia kusanyiko hili usiku wa leo, jinsi ambavyo Wewe umeniongoza katika mambo haya yote, jinsi ambavyo umeniongoza!

152 Nilikuwa ninawazia juzijuzi; si zaidi ya miaka michache iliyopita, nikisimama hapa chini mtaani, na kwa kuwa jamaa yangu ilikuwa imefanya makosa, hakuna mtu angalizungumza nami. Nilikuwa na kiu cha ushirika. Hakuna mtu aliyetaka uhusiano wo wote nami. Wao walisema, "Baba yake ni muuza chang'aa." Basi, Bwana, kwa hiyo hakuna mtu angezungumza nami. Nami nawapenda watu. Bali siku moja nilipoushika ule Waya! Sasa nafikiri, Bwana, sina budi kujificha na kwenda nyikani nipate kupumzika kidogo. Ni nini kilifanya jambo hilo? Si umaarufu wa mtu, si elimu; sina yo yote. Bali ilikuwa ni Wewe, Bwana. Wewe, Bwana. Umenijalia kupiga shabaha, umenijalia kushika samaki wakubwa, kwa maana ulijua nilitaka kufanya

jambo hilo. Umenipa akina baba na akina mama. Umenipa ndugu na dada. Umenipa afya yangu. Umenipa mke. Umenipa familia. Wewe ndiwe Kiongozi wangu, Bwana. Nijalie niushike mkono Wako, usiniache kamwe niuachilie. Kama mkono mmoja ukichoka, nitabadilisha tu mikono. Nisaidie, Bwana.

153 Basi sasa jalia kila mmoja hapa ashike Kamba iyo hiyo ya Uhai, Bwana, Roho Mtakatifu ambaye ndiye Uzima wetu, Mtoa Uzima. Pia jalia atuongoze sote kwenye ile Nchi yenye furaha huko ng'ambo, ambako masumbuko ya maisha yamekwisha na kazi ya duniani imemalizika, halafu hakutakuwako na uzee tena, hakuna watu wanyonge, hakuna usiku wenye uchovu tena, hakuna tena kulia na kuomba, hakuna tena wito wa madhabahuni, lakini tutakuwa vijana kule milele, maradhi na huzuni havitakuweko tena. Hakutakuwa na dhambi tena, nasi tutaishi katika haki ya Mungu katika nyakati zote zijazo, katika Umilele usio na mwisho. Tujalie, Baba.

154 Basi sasa, Baba, kama kuna mmoja hapa usiku huu ambaye hajashikilia kamwe Kamba hiyo ya Uhai, jalia waipate sasa hivi. Pia jalia Roho Mtakatifu ambaye ametuongoza . . . Nami naweza kusema kutoka moyoni mwangu, huku mkono wangu ukiwa juu ya Neno Lako, Yeye daima amekuwa sahihi. Mimi ninakosea mara nyingi. Lakini Yeye yuko sahihi. Naomba kwamba akae nami, Bwana. Naomba kwamba nikae pamoja Naye. Na naomba wengine humu ndani, ambao hawamjui Yeye usiku wa leo, naomba waushike mkono Wake usiobadilika, ili kwamba wapate kuongozwa njiani.

155 Na siku moja tunashuka kuja mtoni. Kutakuwa na ukungu asubuhi hiyo, pia. Bahari ya kale itakuwa inavuma, ule Yordani wa kale, huku mawimbi yakipiga, mauti yakitusonga uhai ututoke. Lakini, Mungu, si—sitaogopa. Nilimaliza jambo hilo zamani sana. Ninataka tu kuitoa ile chapeo, kama shujaa wa vita, nigeuke, niangalie nyuma kote kote njiani nione mahali ile kamba iliponiongoza. Nione nyika yote nilimopitia, na kila sehemu yenye miiba, na kila lundo la mawe nilipochubuliwa, lakini nikiushikilia ule Waya. Kama ulivyosema Wewe, mshairi ndiye aliyesema, "Wengine walipitia majini, na wengine kwenye mafuriko, wengine kupitia kwenye majaribu makuu, lakini wote walipitia kwenye ile Damu." Nami nataka kuuchukua Huu, ule Upanga wa kale hapa ambao umenilinda kote njiani, na kuurudisha kwenye ala Yake, nipaze sauti, "Baba, tuma ile mashua ng'ambo ya pili asubuhi ya leo, naja nyumbani." Utakuwa pale, Bwana. Uliahidi jambo hilo. Huwezi kushindwa.

156 Mbariki kila mmoja aliyeko hapa sasa. Na iwapo hawajui jinsi ya kushikilia Kamba hii, wala hawajaigusa, naomba mikono mitakatifu iinuliwe sasa, mikono yenye haja, mikono yenye shauku, na iguse ile Kamba ya Uhai itakayowaongoza mahali mioyo yao inapotamani, amani kamilifu na ridhaa, raha katika Kristo.

157 Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, kungekuwa na mikono ambayo ingeinuliwa na kusema, "Nijalie. Ushike mkono wangu"? Loo, Mungu awabariki.

> Wakati njia inaanza kuchosha, Bwana wa thamani, uwe karibu,
> Wakati maisha yangu karibu yamekwisha;
> Mtoni nitasimama, iongoze miguu yangu, ushike mkono wangu,
> Nishike mkono wangu, Bwana wa thamani, uniongoze.

158 Kuna mwingine angeweza kuinua mkono wake, aseme, "Bwana, nataka kusikia ule mguso wa Kamba ya Uhai usiku wa leo. Nataka kujisikia kwamba Kristo amenisamehe dhambi zangu, nami nataka kuwa kiumbe kipya tangu sasa na kuendelea"? Mungu akubariki. Kungekuwa na mwingine atakayesema, "Jalia nikuguse Wewe, Bwana. Hebu nijipoteze? Mungu akubariki, dada. Hebu nijipoteze ndipo nijipate, Bwana, katika Wewe." Mungu akubariki. Pia Mungu akubariki wewe. Hiyo ni kweli. "Jalia nijipoteze, Bwana. Jalia nisahau." Mungu akubariki, ndugu. "Hebu mimi . . . " Mungu akubariki, dada. "Hebu mimi nipoteze maarifa yangu yote." Mungu akubariki, dada. Usitegemee mipango ya kujitengenezea. Mfuate Kiongozi, atakuongoza akuingize katika Kweli yote. "Niongoze, Bwana Yesu, niongoze." Mungu akubariki nyuma kule. Loo, kuna mikono mingi iliyoinuliwa, ikitaka wokovu. Basi wakati sisi . . .

159 Madhabahu hapa, huwezi kutoa wito wa madhabahuni, kwa maana watu wameketi kila mahali juu yake. Lakini Yeye yuko papo hapo. Unajua vizuri kabisa, ulipouinua mkono wako, kitu fulani kilitukia moyoni mwako. Yesu alisema, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele." Unamaanisha jambo hilo? Basi kuna kidimbwi hapa kilichojaa maji. Kutakuweko na wakati mwingi kwa ajili ya ubatizo. Na tuombe.

160 Baba yetu wa Mbinguni, ujumbe huu uliovunjika-vunjika usiku wa leo kupitia sauti iliyopwelea, hapana budi Roho Mtakatifu alitoka akaenda mahali fulani. Alienda mahali alipokusudiwa, na wako wengi, Bwana, usiku wa leo, kama kumi na watano ama ishirini waliinua mikono yao, ya kwamba wao wanataka Kiongozi. Wanatambua ya kwamba wanajaribu kujidanganya wenyewe. Wao wanajaribu kusema "Mimi ni sawa," lakini kule chini kabisa wanajua wao hawako sawa. Nao wanataka kukusikia, Bwana. Wao wanamtaka Kiongozi. Wanataka kujiandikisha. Wewe hujai kamwe. Wao wanataka kujiandikisha kwa ajili ya safari hii. Hawajui jinsi ya kufika kule. Hakuna anayejua jinsi ya kuwapeleka kule; ni Wewe peke Yako. Wao wanakuja kwa ajili ya Kiongozi aliyetolewa na Mungu, Roho Mtakatifu. Wameinua mikono yao.

161 Ee Roho Mtakatifu na Kiongozi, shuka juu yao. Samehe kila dhambi. Wasamehe makosa yao. Wachukue uwaingize katika Mwili wa Kristo usiku wa leo, mahali ambapo wanaweza kusikia mkondo wa Mungu ukitiririka kupitia kwenye huo Waya ambao utawaongoza washuke kwenda Yordani, kisha wauvuke Yordani waingie kwenye Nchi ya ahadi. Jalia wafuate moja kwa moja nyuma ya Neno. Neno lilisema, "Tubuni, halafu mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo." Jalia wasijaribu njia nyingine. Jalia wafuate moja kwa moja nyuma ya Neno, kwa kuwa Yeye ndiye atakayeongoza. Hizo—hizo ndizo hatua za kupanda mpaka tunapoweza kumshika yule Kiongozi. Tujalie hilo, Bwana. Naomba wawe Wako. Wako mikononi Mwako sasa, kama tunzo, hakuna mtu anayeweza kuwatoa. Ninaamini ya kwamba utawachukua, kama watu waliookoka. Ninaamini ya kwamba wao waliinua mikono yao, wasingeweza kufanya jambo hilo wenyewe isipokuwa Kitu Fulani kilinena nao. Huyo alikuwa ni Wewe, ewe Roho Mtakatifu na Kiongozi.

162 Wao wanaona ile saa ikikaribia, ukungu unakuja juu ya nchi, kanuni kuu za imani na—na kadhalika vinaungana pamoja, makanisa yanaungana, yakikusanyika pamoja. Pia, Ee Mungu, jinsi wanavyojaribu kusema, "Wote walio na jambo la kigeni hawana budi kuondoka hapa waende huko Alaska." Na mambo haya yote wanayotisha, si jambo jipya kwetu, yule Kiongozi mkuu ametuonyesha jambo hilo katika njia ya Neno. Tunapitia tu sehemu hiyo Yake.

163 Baba, Mungu, ulinena nao usiku wa leo, nami nakupa Wewe hao kama tunzo la Neno. Katika Jina la Yesu.

164 Naam, hapa kwenye dawati, Baba, kuna leso, ni za wagonjwa, watoto fulani wachanga, labda, mama fulani, dada fulani, ndugu fulani; hata vipini vidogo vya nywele vimechomekwa kwazo. Na sasa ninazishikilia juu karibu nami. Naam, tunafundishwa katika Biblia ya kwamba walichukua kutoka kwenye mwili wa Paulo leso na aproni, na wagonjwa waliponywa, pepo wachafu wakawatoka watu. Sasa tunatambua, Bwana, ya kwamba Paulo alikuwa mwanadamu, alikuwa mwanadamu tu. Lakini ilikuwa ni ule upako wa Roho Mtakatifu uliokuwa juu yake ambao ulizibariki zile leso, na imani waliyokuwa nayo hao watu ya kwamba yeye alikuwa mtume Wako. Sasa Paulo ameondolewa kwetu, bali si yule Kiongozi, Yeye yungali hapa. Pia, Mungu, naomba ya kwamba utazibariki leso hizi, na jalia yule Kiongozi awaongoze kwenye mahali pale, kule kujisalimisha kabisa.

165 Tunaambiwa tena ya kwamba wakati Israeli walipokuwa wakimfuata Kiongozi wao, nao wakafika moja kwa moja kule Yordani, moja kwa moja (hasa) kwenye Bahari ya Shamu. Wakiwa katika wajibu wao kabisa walisimamishwa, ndipo Kiongozi akawaongoza kule chini. Ati nini? Kuonyesha utukufu Wake. Basi wakati matumaini yote yamekwisha, ndipo Mungu

aliangalia chini kupitia ile Nguzo ya Moto, na hata maskini Bahari ya Chumvi ikaogopa na kurudi nyuma, ndipo njia ikafanywa ili Isreli waipitie kwenda kwenye nchi ya ahadi.

166 Kweli, Bwana, Wewe ungali Mungu yeye yule. Watu hawa labda ni Wakristo, labda wako moja kwa moja kwenye wajibu wao, bali wameletwa kwenye mahali hapa pembeni ambapo maradhi yamewakaba. Angalia chini kupitia Damu ya Bwana Yesu usiku wa leo, Ibilisi huyo aogope, atarudi nyuma, nao watoto Wako watavuka waingie kwenye ahadi ya afya nzuri. Tujalie, Baba. Ninazituma kutoka kwenye mwili wangu hadi kwenye miili yao, katika Jina la Yesu Kristo.

167 Ninaliinua kusanyiko hili mbele Yako, kwa imani ninawachukua moja kwa moja hata kwenye madhabahu yenye utukufu ya Mungu kule juu Mbinguni. Kwa kila shauku ya maradhi, cho chote walicho nacho ambacho si sawa, cho chote kilicho kibaya katika maisha yao po pote pale, Mungu, wasafishe, wafanye wawe Wako. Waponye, Baba. Na Nguvu zilizomfufua Yesu kutoka kaburini, ziihuishe miili yao inayopatikana na mauti na iwafanye viumbe wapya katika Kristo. Wape afya njema na nguvu wapate kukutumikia.

168 Nikumbuke, Ee Bwana. Mimi ni mtumishi Wako. Nisaidie, nikisimama nikiwa ninahitaji maombi. Nami naomba ya kwamba Roho Mtakatifu atatuongoza na kututumia, na kutuongoza hata siku ile tutakapomwona Yesu Kristo uso kwa uso katika kule Kuja Kwake kwenye utukufu tutakapomlaki hewani katika Kunyakuliwa. Katika Jina la Kristo tunaomba. Amina.

Ninampenda, Ni-. . . (Nanyi je?)
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

169 Naam, kama hampendani ninyi kwa ninyi ambao mmeonana, mtampendaje Yeye Ambaye hamjamwona? Basi tunapoimba *Nampenda*, hebu tumpe mkono wa upendo jirani yetu kwa furaha sana.

Nampenda, . . .
[Ndugu Branham anapeana mikono na wale walio karibu naye. Kisha anasema, "Mungu akubariki, Ndugu Neville."—Mh.]
[Kusanyiko linaendelea kuimba.]
Mtini Kalvari.

Hebu sasa tumwinulie Yeye mikono yenu.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

170 Kwa ajili ya wimbo mzuri, mngetaka kuusikia mmoja? Nasikia tuna mwijilisti kiongozi wa nyimbo hapa kutoka Indianapolis. Ninaamini yeye huimba kwenye Maskani ya Cadle. Hiyo ni kweli? Vema, bwana. Hapo ndipo mahali pake kwenye Maskani ya Cadle. Ni wangapi wanamkumbuka E. Howard Cadle? Loo, jamani! Mungu na aipe raha nafsi yake ya thamani. Ndege mwimbaji wa angani, mwanamke niliyependa kumsikia akiimba, vizuri kuliko karibu mtu ye yote niliyewahi kusikia akiimba maishani mwangu, alikuwa ni Bi. Cadle, akiimba, "Kabla hujaondoka chumbani mwako asubuhi ya leo, ulikumbuka kuomba katika Jina la Kristo Mwokozi wetu, kama Ngao leo?"

171 Moja kwa moja upande wa pili wa barabara pale asubuhi moja, katika kibanda kidogo cha kale chenye vyumba viwili, niliamka, nilikuwa ninaingia nikawashe moto. Jiko halingewaka. Nami nikajaribu kuliwasha, ndipo upepo ukashuka, ukazima kitu hicho usoni mwangu. Na kulikuwa kuna baridi, nami nilikuwa karibu nimeganda kwa baridi. Na umande kila mahali sakafuni, nami miguu mitupu; nikijaribu kuliwasha jiko hili la kale la bati, lenye bomba ndogo la jiko. Nami nilinini hii tu. . . Mimi na Meda tulikuwa ndiyo kwanza tufunge ndoa hivi karibuni. Nami nilikuwa ninajaribu, kuni zile za kale zilikuwa zimelowa maji na hazingeungua, nami nilikuwa nimeketi pale, nikawaza, "Loo, jamani! Nitajaribu hilo tena." Ilinibidi kwenda kazini, huku ninapulizia lile jiko la kale namna hiyo. Ndipo nikanyosha mkono wangu nikafungulia redio, naye akaanza kuimba, "Kabla hujaondoka chumbani mwako asubuhi hii, ulikumbuka kuomba," nilianguka tu sakafuni, "katika Jina la Kristo Mwokozi wetu, kama Ngao leo?"' Loo, jinsi ninavyopenda kumsikia mwanamke huyo!

172 Nitakapovuka ule mto siku moja, ninaamini nitamsikia Bi. Cadle ameketi kule. Mwajua, daima nimefanya miadi. Upande huu wa mto, kuna ule Mti usiokauka, mwajua, mti wa Uzima; na upande wa pili wa mto, kuna kwaya ya Malaika inayoimba usiku na mchana, maana hakuna usiku kule, wanaimba siku nzima, mnaona. Nitajipatia mahali na niketi tu kitako na kuisikiliza. Ninaamini nitamsikia Bi. Cadle kule akiimba.

173 Mungu ambariki ndugu yetu. Nilisahau jina lake. Ni jina gani, ndugu? Ndugu Ned Woolman atawaimbia sasa. Ndugu Woolman, tunafurahi kuwa pamoja nawe usiku huu.

*Kiongozi* SWA62-1014E
(A Guide)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, 14 Oktoba, 1962, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Hii tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 1994 na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1994 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani  kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org